

CONSTITUTION OF KENYA REVIEW COMMISSION

(CKRC)

VERBATIM REPORT OF

CONSTITUENCY PUBLIC HEARINGS,

BARINGO NORTH CONSTITUENCY,

HELD AT KABARTONJO CHIEFS OFFICE

ON

3rd JULY, 2002

**CONSTITUENCY PUBLIC HEARINGS, BARINGO NORTH CONSTITUENCY, HELD AT KABARTONJO
CHIEFS OFFICE ON 3RD JULY, 2002**

Present

Com. P.M. wambua
Com. Zein Abubakar
Com. Pastor Zablon Ayonga
Com. Hon. Phoebe Asiyu

Secretariat Staff in Attendance:

Fatuma Jama - Programme Officer
Makomere Wambeyi - Asst. Programme Officer
Lydia Moraa - Verbatim Recorder

The meeting started at 10.20 with a prayer. Com. Wambua in chair.

Speaker: Shughuli ya leo. Na kabla hatujafanya jambo lolote, ninaomba Reverend Chirchir aje atuongoze kwa maombi tafadhali. Na tusimame zote.

Rev. Chirchir: Tuombe pamoja. Mungu Baba wetu, Mungu muumba, na mlizi ya wote tunakushukuru asubuhi hii kwa uongozi wako bora, asante kwa kuanziza kazi hii, asante kwa yale yametendeka na Baba tunataka kujikabidhi mikononi

mwako wakati huu. Tunakushukuru kwa kuongoza na kulinda wale wanaongoza kazi ya leo. Baba tunajua hii ni kazi ya maana sana ambaye nchi yetu itakuja kutegemea; sisi wakati huu na hata kwa watu wa siku sijazo. Baba tunataka utuongoze na utusaidie tujadiriane na tuchukue kila kitu kwa makini. Baba tunakubuka wale wanaendelea kwa sehemu tofauti tofauti kwa jamhuri yetu ya Kenya. Baba upate kuongoza na hii wewe mapenzi yako ipate kujulikana ili nchi hii ipate kwendelea kwa amani na ufanisi wa maendeleo. Tunakushukuru kwa mambo hayo yote katika jina la Yesu aliye bwana na mwokozi wetu. Amen.

Speaker: Basi, asante reverend, wakati tunapoendelea, nawaomba ya kwamba kila mtu ajiandikishe tafadhali na mahali pa kujiandikisha itakua ni mahali pale, hata kama hutakua na nene ambayo ungependa kusema, wewe uende tu ujiandikishe basi. Kwa nafasi niliyonayo nitamkalibisha mwenyekiti wa committee wa North Baringo constituency ambaye ni Royeta. Karibu Royeta.

Royeta: Commissioner Zablon Ayonga na tena ni chairman na Commissioner Asiyo, Commissioner Abubakar, Commissioner Wambua, paradiyo kamati ya Katiba ya constituency ya Baringo North. Yangu tu ni kuintroduce wale kamati ya ... kujeni pande hii tafadhalini. Kuja pande hii halafu muende kuketi. Commissioners, nitawaonyesha wale walifanya kazi hii ya Katiba at monitoring the civic education providers kwa kila division. Hawa .. kuna wacomitte yete mwingine ako nje? Bwana chairman, kuanzia hawa akina mama, huyu ni Rodha Kiplangat, mama mwingine ni Presca Chepsengei, hawa wanaakilisha Kabartonjo division. Kijana huyu ako na suit nyeusi anaitwa Erick Arare kutoka Partambo division. Anaakilisha youth kwa Katiba. Pastor John Chebeti – yeye ni programmer wa leo, Bwana Commissioner, yeye anaakilisha Religion – Dini kwa jumla kwa Baringo constituency. Yule anafaa Chesero, tena vile vile pastor anatoka Kabartonjo division, sio ya Chesoro Bwana commissioner ni kutoka Kabartonjo division inaitwa Chepchesoro – jina ingine ni Lang’olat. Na commissioners, wale wengine bwana chairman tuko na bando labda tuko watatu, tuko na mwingine anaitwa Labad kutoka Parwesa division bando ingia. Na kuna mwingine aliomba apology Natachemi Siala ameenda kwa seminar anaakilisha Kabartonjo division. Nafikiri ni hayo tu sina Na co-ordinator tuko na representative ya coordinator office. Kwa haya machache kwa sababu nyinyi hamtaki maneno mingi, mimi tu nashukuru nakaribisha commissioners, ni nasema asante sana kwa constituency yetu ya Baringo. Tumefanya kazi, commissioners tumefanya, tumefanya kila mahali. Tumejaribu kutembelea kila location, wacha ata tarafa,

tumeenda kwa kila location kupeleka kazi hii ya Katiba. Kwa hivyo _____ (inaudible) kama jana Bwana chairman ulijionea. Tulitetea kila corner na tunaamini tumefaulu na tulisaidiana na Administration. Unajua saa ingine, unajua pande hii lazima tusaidiane na watawala kwa sababu ya milima, communication ya barabara saa ingine na security saa ingine kwani imejaa Wapokot. Wanalalamika juu ya vita ya kuimba ng'ombe, ng'ombe. Kwa hayo machache mimi sina maneno mengi, ninakalibisha DO ya _____ (inaudible) Baringo North ili akalibishe wageni na akalibishe Chairman sana. Karibu bwana DO.

DO: Basi chairman ya kikao hiki pastor commissioner Zablon Ayonga, commissioners ambao mumeandamana nao, yangu ni kuchukua nafasi hii kidogo kuwakalibisha katika tarafa hii ya Kabartonjo ambao tunatarajia watu kutoka divisions mbili – Barweza division and Kabartonjo division.

Barweza division iko na locations tatu, na Kabartonjo division locations tano. Kwa wakati huu viongozi ambao walichaguliwa kutoka mjumbe, councillors, naamini watakuwa nasi siku ya leo. Kwa watu wetu wa Kabartonjo na Barweza, langu tu itakuwa matatu; moja ni kwamba tujaribu tuongee mambo ambayo inahusu taifa kwa ujumra. Tusiangalie zile shinda zetu za hapa kwa mlango, tuangalie nchi kwa ujumla, ukipatiwa dakika tano, sema jina lako na useme ile unataka, usiamke na kusema bwana chairman, councillors, chiefs, wazee wa mitaa, chairman ya _____, nursery, nachukua nafasi hii kwetu ni salama haijanyesha, iko nini, No! Nasijui, ukiwa na memorandum, usitusomee kila kitu, highlight please and hand it tuokoe wakati. Kwa hivyo mwenyekiti utakuta wazee pia wamekuja hapa na watatoa maoni yao kwa lugha yao. Bila kupoteza wakati ninarudishia chairman ili tuanze kikao hiki mapema. Tumekuja nje hapa kwa matumuni ya kwamba, tuwe wazi, hakuna kitu ambayo tunaficha, lakini hali ya anga ikibadirika, tutamia hiyo hall. Tumekuja hapa nje kuonyesha kila mwananchi kwamba, hii commission haina chochote ya kuficha. Kwa hivyo hali ya anga ikibadilika tutatumia kule dani. Basi, kwa sababu leo hatuna makofi, nini na nini makofi tatu ya kilo.

Hapa la mwisho, hapa ni kortini, this is a commission, hata ukisikia matusi, usicheke. Take it as a court. Hakuna kushangilia, hakuna kuuliza maswali, lete vile ungetaka. Asante.

Com. Pastor Zablon Ayonga: Asante Bwana DO, nataka kuwasalimu nyote kwamba Change tubu, tumefurahi kufika upande wenu wa Kabartonjo na tunashukuru bwana DO kwa makalibisho, tumeshukuru, bwana mwenyekiti wa 3Cs kwa

kutukalibisha, tunajua imekuwa kazi ngumu kwenu, kuweza kumobilize watu ili waweze kuja katika kikao hiki na jinsi ambavyo bwana DO amesema, leo sio siku ya maswali. Leo ni siku ya maoni yako ambayo unayotambua hivi ndivyo ungetaka Katiba ya Kenya iwe. Maneno ya mastory vile jinsi mambo yalifanyika, hivi na vile, ndipo uje kutwambia point yako huko mwisho, hio si haja. Tunataka ugongwe point ile ambayo umetaka, na tunataka utwambie suruhisho. Si kwamba unatwambia, sasa nyinyi commission mwende muangalie habari hiyo. Habari hiyo ni wewe unaangalia, sisi tutabeba habari ili ambayo wewe umeandalia. Tena hata mtu kama amesema point ambaye imekuungia, hatutaki kupiga makofi, kule kotini mkienda mnapiga makofi? Hakuna. Tunataka tu tuwe na ukimia, kila mmoja atapewa nafasi yake ile ambayo itatoa maoni yake.

Na pia tungelipenda kila mmoja anapoambiwa dakika zako zimekwisha ili upatie na mwingine nafasi ni heri utii. Usiseme mimi ngoja, ongeza mimi dakika, unaposema hivyo, unataka kusema ni wewe tu uko upande huu. Hawa wengine wote wako hapa wamekuja watoe maoni, kwa hivyo ukiambiwa dakika zako zimekwisha, tafadhali upoe. Temeelewana? Sasa kabla hatujaenda kuwapa yale mambo ambayo mtafuata, nataka kuchukua fursa hii kwa kuweza kuintroduce kwenu commissioners ambao tumekuwa hapa na office staff ambao tumekuwa nao. Nitawapa nafasi commissioners baadaye wawasalimu lakini kwa kutaja, mkono wangu wa kushoto ni commissioner B. Asiyo ambaye nina ukweli kwamba wengi wenu wanamjua alipokuwa mwanabunge na sasa yeye ni commissioner. Atawasalimu baadaye. Na hapa karibu nami ni bwana Abubakar Zein ambaye ni commissioner, nitampa nafasi atakuja kuwasalimu na kule mwisho ni commissioner Paul Wambua. Naye pia atawasalimu baadaye. Hata kwa office tumekuwa na Programme Officer ambaye ni Bi. Fatuma na huyu ndiye kiongozi wa programme yetu hapa na amekuwa pia na wengine watatu, moja atakuwa ni Makomere ambaye yeye atakuwa anaandika, anaandika kama machine lakini hata kama anaandika, kuna Bi Moraa hapa, ambaye yeye naye anatega na kanda ili neno lisipotee. Hata kama unakohoa, kikohozi chako tutachukua. Kwa hivyo hakuna neno la mtu litakalopotea kwa kuwepo hapa. Sisi commissioners pia tutakuwa tunaandika lakini mara nyingi utaona tunasikiza. Usije ukaseme bona ninaona yule commissioner haandiki maneno yangu. Kuna naye anaandika, kuna naye anashika maneno yako kwa kanda. Kwa hivyo hakuna kitu cha mtu hapa kitakuja potea, tunataka mkisema useme dhaili, unajua zile siku zingine mtu anaweza kusema, nikisema DO yuko hapa, nafikiri baada ya hii mkutano nitashikwa juu juu au chief yuko hapa, au nani yuko hapa, hiyo leo hakuna. Nyinyi nyote mmefunikwa na ile blanket nzuri ya commission, kwamba hakuna atakayeshitakiwa kwa maana alitoa maoni yake. Tumeeleana? Kwa hivyo leo ni siku ya uhuru, na useme yale unayotaka. Ili nisije nisahau, wacha wacommissioners wawasalimu na wakishawasalimu leo

ambaye atakalia hiki kiti changu, atakuwa commissioner Paul Wambua, ndiye ataendesha hiki kipindi. Kwa hivyo wacha kwanza msalimiwe. Mama Asiyo,

Com. Phoebe Asiyo: Asante sana commissioner Pasor Ayonga kwa kunipa nafasi ya kuwasalimia watu wote, wazee na vijana ambao wamefika hapa Kabartonjo ili kutoa maoni juu ya Katiba mpya. Najua mnafahamu kwamba Katiba ndio amri kuu kabisa. Ndio sheria ile kumbwa zaidi ya sheria yote. Na pia mnafahamu kwamba hii Katiba tulionayo kwa wakati huu ni Katiba ile ilitolewa ulaya na imelekebiswa kama mara tharadhine na nane hivi. Sasa ni kusema wanakenya wenyewe (nyinyi wenyewe) leo mnajenga nyumba mpya ya Kenya. Ndio mtajua kijana anakaa upande hii, mzee nyumba yake itakuwa pale, ng'ombe watakaa namna gani, jee mambo ya kuheshimiana itakuwa vipi? Sheria za Kenya zitakuwa namna gani? Ndio sasa tutajenga nyumba mpya na watu wa Kenya wenyewe. Na mimi ninashukurani sana kwa watu wa Kenya kufikia wakati huyu wa kusema tutengeneze Katiba. Mnajua kwa Africa, hata nchi zingine, Katiba imetengenezwa kukiwa na vita, au kukiwa na msukosuko mbaya sana – crisis mbaya sana ya nchi mzima. Watu wanashindwa kuishi vizuri, halafu wanakimbilia wanasema tukae chini tutengeneze Katiba mpya. Ni chache sana itengeneze Katiba mpya kama President yuko na yeye aseme tutengeneze Katiba mpya. President wachache sana wa Africa wanafanya mambo hii hapa. Ni mzuri kusema ukweli, wachache sana wanakubali – kama wao bando wanaishi – kusema Katiba iandikwe mpya. Mimi nikisema hiyo ni mzuri maana mimi ni mwanabunge miaka mingi, najua mambo ya siasa ya Kenya. kwa hivyo tunapeana shukurani kwa mambo haya, kwa serikali, kwa mzee mwenyewe, kwa watu wa Kenya kukumbali kwamba itengenezwe Katiba mpya kama President yetu bando yuko mzima na yuko kwa kiti. Na tutengeneze Katiba ambayo itaweza kuleta urafiki kati ya watu wa Kenya wote ili tuishi kama watoto wa mtu mmoja. Maana Mungu hakuwa mjinga kuweka sisi pamoja. Alikuwa na sababu yake ya kuweka sisi wote kutoka pahali ya Mombasa, mpaka milima hii yote ya Baringo ati sisi ni watu wa nchi inaitwa nchi ya Kenya moja. Mungu alikuwa na sababu kubwa sana. Kwa hivyo Katiba hii kama tutafulu kuleta urafiki kwa ajiri ya Katiba hii, itakuwa kitu ya maana sana. Lakini mtupatie mawaidha, mtupatie fikira yenu, serikali ambayo itakuwa namna gani, je vijana, wazee, mali ya uma na kila kitu kitakuwa je. Ninajua tutapata hekina kutoka kwa wazee mbao mimi naona hapa. Nimeshukuru sana sana kwamba mmefika na kwamba tutaongea kama watu wazima ili tutoke na mambo itatusaidia kufanya Katiba. Nakushukuru mwenyekiti kunipa nafasi ya kusalimia watu hawa, na mimi pia ni mtu wenu hapa, kijana yangu alitafuta wasichana Kenya yoote akaja akaoa hapa kwenu, hata mimi ni sengee hapa. (laughter).

Com. Pastor Zablon Ayonga: Sasa mimi naona hapa tuko ugeni tena ugeni mkubwa sana kwa maana kama mama mlitafuta msichanaaa mpaka mkaja kupata yapa, tukimaliza kikao hiki, si mama atalala? Tunaeleana? Haya, wacha msalimiwe hapa na commissioner Zein Abubakar.

Com. Zein Abubakar: Habari ya asubuhi? Kila wakati ninapokuwa safarini nikiwa nimeandamana na mzee Ayonga na Mheshimiwa mama Asiyo, huwa mimi najifunza mambo mengi na ninapata busara kubwa nyingi. Na kile mnapozungumza na kusikiza maoni ya wakenya, huwa najifunza mambo kama hayo. Kwa hivyo, kulingana na mira na desturi zetu kule Mombasa, ikiwa mambo mazuri kama haya aliyosema mama, nikianza na mimi yangu nitakuwa nimeyaharibu, kwa hivyo mimi ningependa tu kuwasalimia na kuwaambia kwamba nina furaha kubwa kuwa na nyinyi na tunashukuru mmeweza kuitikia mwito wa kuja kutoa maoni ili kulekebisha Katiba yetu. Asanteni sana.

Com. Pastor Zablon Ayonga: Sasa wacha msalimiwe na Bwana Paul Wambua.

Com. P.M. Wambua: Change tu? Mimi kwa kawaida wazee wakizungumza huwa sipendelei kuongezea maneno, ni kama dugu yangu hapa Zein alisoma yale niliyolikuwa nataka kusema. Nafikiria kwa kuwa niko karibu naye. Kwa hivyo sitaongezea yale mliyoyasikia kutoka kwa commissioners Zablon Ayonga na Mama Asiyo. Ni yale yale ambayo yanafaa. Kwa hivyo kwangu ni kusema na washukuru nyote kwa kufika, natarajia ya kwamba kila mmoja wenu atayatoa maoni yake kulingana na vile angelipenda Katiba yetu iwe. Kwa hivyo mjisikie mko huru kusema yale yote ambayo yako moyoni, yako kwa kichwa yenu halafu tutayapokea na Katiba tutahakikisha ya kwamba maoni yenu yatakuwa yameingizwa katika Katiba. Kwa hivyo asante sana Bwana mwenyekiti kwa kunipa nafasi kuwasalimia hawa dugu zetu.

Com. Pastor Zablon Ayonga: Asante, baada ya hayo, tuliwaambia kwamba nimemuuliza huyu commissioner Bwana Paul Wambua ili aweze kuwa mwenyekiti kwa kikao hiki. Yeye atawapa kwanza taratibu ya jinsi tutafanya, jinsi ambavyo unatakiwa ufanye, na jinsi ambavyo mkutano huu utaendelea. Kwa hivyo kwa sasa ninampa microphone na atawaeleza na ataongoza kikao hiki.

Com. P. M. Wambua: Asante sana mwenyekiti, tutafuata taratibu kama ifuatavyo:-

Unaweza kuja hapa kutoa maoni ukiwa umeyaandika – written memorandum, kama uko na maadishi na hutaki kuzungumza ama kuongezea yale ambayo umesema, tutayapokea na tutaandikisha hapo na tutaenda kuyasoma. Ikiwa ungelipenda kuongezea machache ama kumlika yale ya mhimu kama vile mwenyekiti alivyosema, basi muda wako utapungua kidogo halafu tutakupa nafasi tu ulenge yale ya muhimu halafu umuachie mwenzako nafasi. Tunatarajia ya kwamba watu watakuwa wengi, kwa hivyo ukija hapa kuzungumza, lenga yale ambayo yanafaa kuhakikisha ya kwamba Katiba ambayo itaandikwa inaofaa. Kwa hivyo tutafuata taratibu wale ambao wamejiandikisha ya kwamba kuna orodha ambayo imeandikwa, majina yamepeanwa, tayari tuko na watu 36. Tutawaita wale ambao walijiandikisha kwanza halafu itafuatana hivo hivo. Lakini sisi tuko na haki, ikiwa kuna mtu amefika hapa na ni ngojwa, ama ni mama mzito, ama ni mama, ama ni mzee, ama awe ni mtu ana kilema, awe ni kilema tutampa nafasi, tuna haki ya kumpa nafasi kwanza atoe maoni halafu aende. Kwa hivyo ukiona pengine mtu amekuja hivi karibuni na wewe ulikuwa hapa tangu mwanzo, halafu tukampa nafasi, ujuwe kuna sababu lakini tutataja kwa nini tunampa hiyo nafasi. Na hivyo ni taratibu ambazo tumetumia kila pahali tulipofika.

Baada ya kutoa maoni yako, tutahitaji ujiandikishe huko kwamba ulifika na ukatoa maoni halafu jina lako utaweka sahihi wako hapa wale ambao wanatakiwa waandike. Kwa hivyo bila kuharibu wakati na pia la mwisho, commissioners wako na haki ya kuuliza maswali kama kuna neno ambayo halikuweleweka, tuna haki kama commissioners kuuliza ufafanue lakini hatutakubali kuwe na mjadara. Wewe ni kusikiza vile watu wanasema, wao watatoa maoni yao na we utatoa maoni yako. Hata ikiwa hukubaliani na hao, maoni ni yao au ni ya wao, kwa hivyo utoe yale yako. Sio ati utakuja kujibu vile mwenzako amesema, apana, toa maoni yako. Hata ikiwa ni tofauti kulingana na wale walivyozungumza mbele yako. Kwa hivyo tutaanza maanake muda hatuna sana, kwa hivyo nimekubushwa kwamba unaweza kutumia lugha yeyote, kizungu, kimombo, unaweza kutumia kiswahili na ikiwa uko na shida kuzungumza lugha hizo mbili, tunaweza kukupa nafasi uzungumze na ile tunaita mother tongue. Hapa tuna Ntugeni, hiyo pia tunaelewa. Na wale ambao hawaelewi, tuko na mkalimani hapa atatafusiri atatwambia yale umesema halafu yatanaswa. Kwa hivyo tuanze mbele kabisa niko na Mariko Cheboiwo, Mariko Cheboiwo, Mariko tafadhali fika hapa mbele, taja jina lako, tunataka utaje ndio linaswe halafu utupatie maoni yako. Nahakikisha hutapitisha dakika kumi maanake ... kwa hivyo taja jina mzee halafu uendelee.

Mark Cheboiwo: *Kainenyun ko Mariko Cheboiwo.*

Translator: Jina lake ni Marko Cheboiwo.

Mark Cheboiwo: *Ang'alanen kutinyun.*

Translator: Ataongea kwa lugha yake.

Mark Cheboiwo: *Ng'olyot nebo tai ko koboch kenam katyaknatet agoi raini,*

Translator: Jambo la kwanza, tangu tulipopata uhuru mpaka wa leo

Mark Cheboiwo: *kokiteb emoni eng' kalya, kimochekoteb ku non.*

Translator: tumekaa kwa amani na tunataka iendelee hivyo.

Mark Cheboiwo: *Ne bo aeng', momeche ng'alekab ukabila.*

Translator: Ya pili, sitaki mambo ya ukabila.

Mark Cheboiwo: *Komoche ketebi ku yu kitebsot che bo keny.*

Translator: Nataka tukae kama vile tulivyokuwa tukikaa tangu zamani.

Mark Cheboiwo: *Nebo somok ne bo let,*

Translator: Jambo la tatu na ni la mwisho,

Mark Cheboiwo: *Chang' lagok betusiechu en emoni bo Kenya che monget chi kwanisiek ole mi kamanik.*

Translator: Kuna watoto wengi ambao wa Kenya hii ambao hawajulikani wazazi wao, baba na mama.

Mark Cheboiwo: *Kimoche keib ng'alecho koba Bunge keng'alal ngiborchi lagochu.*

Translator: Tunataka hayo maneno yapelekwe kwa bunge tujue tutawafanyia nini hawa watoto.

Mark Cheboiwo: *Korok ng'alekyuk ane amu kemwa kele makimoche ng'al chechang'.*

Translator: Mambo yangu yameishia hapo kwa sababu umesema hatutaki maneno mengi.

Com. P. M. Wambua: Asante sana, asante sana, jiandikishe hapa mzee Cheboiwo. Na wale watakaofuata tafadhalini fuata mtido ni huo huo sasa. Dakika ni tano, sasa zimepungua kutoka kumi. Amundanyi Kipkulei, tufuate mtido wa Cheboiwo, dakika tano tu, hata kama ni mbili pia maliza maneno yawe machache.

Kipkulei Amndany: *Ane ko Kipkulei Amdany ochome ngalechu bo rani ole keyai amu kaming'inetaabkei*

Translator: Mimi Kulei Amundanyi nataka maneno ya leo tufanye kwa unyenyekefu.

Kipkulei Amndany: *Ne akwang'e kityo ne muo kityo mi ki achek olipokeny keiye komen che kibo gaa, rani kisor kumik chebeny che mwochi serkali kole notobul bunu kiyai sortolak chi lemei en barabara.*

Translator: Jambo linalo nishangasha sana ni kwamba zamani tulikuwa tukinywa pombe ya nyumbani na kwa wakati huu kuna pombe aina mingine mingi baya ambayo inamaliza watu wetu barabarani. Nataka serkali itupilie mbali.

Kipkulei Amundanyi: *ago komen cho ko che kosoru ak keado en dukani.*

Translator: Na hayo pombe yaliingia tu hivi majuzi na yanauzwa dukani.

Kipkulei Amundanyi: *ko mokinget so kebenet ne bunu*

Translator: Na hatujui ni pango gani pombe hii imetoka.

Kipkulei Amundanyi: *aginye serkali oker kebenet ne bunu amache asorta chile ketolek eng' barabara*

Translator: Nataka niambie serkali ifunge hiyo pombe ambayo inamaliza watu barabarani. Sasa mimi sina maneno mengine.

Kipkulei Amundanyi: *Unon, mele atotinye alak chechang' kemwoe kele keyai Katiba ni ak koribech agoi tun, ak korib lagokyok amu ane a chi boiyon ne kokose redio che bo sang'*

Translator: Jambo ninalitaka tu ni kwamba hii Katiba tuiunde na itulinde na ilinde watoto wetu mpaka miaka zijazo kwa sababu mimi ni mzee na ninasikia radio ya hata mambo ya nje.

Kipkulei Amundanyi: *Ko countries chebo Afrika matinye kalya*

Translator: Katika constinent ya Africa vijinga haina amani.

Kipkulei Amundanyi: *Ko Kenya achek ketinye kalya*

Translator: na sisi Kenya tuna amani.

Kipkulei Amundanyi: *Kemoche koteb kalyani agoi tun. Kirok chichuk.*

Translator: na tunataka amani hii ihudumu milele. Asante.

Com. P. M. Wambua: Asante sana Mzee Kipkulei. Umetajaaa... ngojea kidogo mzee. Ametaja pombe ya kienyeji ambayo ilikuwa inatengenezwa hapa awali, angelipenda iendelee ama angelipenda iwe aje?

Kipkulei Amundanyi: *Aa, moendeleani kikerker chon kobek.*

Translator: Anasema pombe ya kienyenji isiendelee, ifungwe.

Kipkulei Amundanyi: *kimwoe chu kioldoi en tukasiek, chon mi kartasit ne teno.*

Translator: Anazungumzia juu ya hii iko kwa duka iko kwa makaratasi.

Com. P. M. Wambua: Asante sana mzee, tumeyasikia. Thank you very much. Jiandikishe hapa tafadhali. Sasa tumuite Naftari K. Chelagat. Hayuko? Endelea, taja jina tafadhali na utoe maoni.

Naftari Chelagat: I salute you commissioners, my names are Naftari Chelagat. My proposals: I seek to introduce a system that secure proper distribution of power. I believe I have a proposal federal system of governance as the only political system suitable and acceptable to the people of Kenya. Centralism will bide Kenyan external unit with its internal diversity since preserving the regional diversity is the traditional _____ of federal system. The federal system leaves room for experiments on a smaller scale and for competition amongst states. A single state may for instance try informative methods in _____ which may later service a model for nation quite reformed.

Preamble: I proposal that the new constitution should contain a preamble that would summarize the _____ side of the constitution and common calls for the Kenyans. I suggest the following preamble: In the name of Jehova Jire, we the people of the republic of Kenya endurance in the guidance of the Almighty God that our forefathers, fought for independence and guided by the said Almighty God who will also guide to the reviewing of the constitution and their substicle in amendment thereafter wish to reconstitute Kenya into a very close sovereign democratic republic republic to secure to all its citizens, their religions, their rights, do hereby adopt enact and keep to ourselves this federal constitution.

The Coalition: I propose that the open chapter of the constitution should declare that Kenya is of sovereign federal republic. The federal republic will be comprised of 8 regions, that is Central, Coast, Eastern, North Eastern, Nyanza, Rift Valley, Nairobi and Western.

Supremacy of the constitution: The supremacy of the constitution must be maintained that it has to be the supreme of the federal republic of Kenya and in any other law that may contradict it shall be void to the extent of that particular inconsistency.

Interjection

Com. Wambua: Naftari, let me guide you, if you read that memorandum, it will take you 20 minutes, please highlight what is important, you have three minutes to go, highlight what is important because we are going to read that memorandum in detail in Nairobi.

Naftari Chelagat: Thank you. The proposals contained in this paper are set out in a summary form, I believe the commissioners the expartees have an ability to paint a clear picture of the governmental strategy structures proposed herein. What remains for the commission to conjunct the proper and material worth and phrases to come up with a comprehensive document that encombases the above proposal. I believe the federal structure system is the only political system which can solve them mental problems facing Kenyans. Thank you.

Com. P. M. Wambua: Thank you very much, we will read that memorandum in details Bwana Naftari, so please record it there and give it to us. Tumuite Reverend Z. C. Chirchir.

I can see you have a written memorandum, please highlight the key points.

Rev. Z. C. Chirchir: My names are Reverend Zacharia Chirchir, chairman Africa Inland Church Baringo North Church _____. The Bible says the light of the body is the eyes. If therefore your eyes are good your whole body shall be full obliged but if your eyes are bad, your whole body will be full of darkness. Mathew 6: 22-23 in the same way the light of our country is its contribution and if its contribution is good the whole country will be full of light and vise versa.

Because I have written document let me just quote another verse and then I will just hand over right away. Regarding the extension of parliament and the completion of the new constitution, the bible says, no one patches up an old goat with a piece of new cloth for the new patch will shrink make an even bigger hole in the coat nor does any one pour new wine into used wineskins for the skins will pass the wine will pour out and the skins will be ruined. Instead, new wine is poured into fresh wineskins and forth will keep in good conditions. Thank you very much.

Com. P. M. Wambua: Thank you very much Reverend for being brief and also inciting the Bible. Thank you very much, register yourself there and let us have the memorandum. Joshua Kipkitor. I can see Joshua you have a written memorandum, please be very brief, summarize; we will read the memorandum in Nairobi.

Joshua Kipkitor: My names are Joshua Kipkitor from Ngantar Pastrol Parish, Baringo North constituency. Sasa

tumeandika na vile tumeandika, kwanza tumeandika introduction na tukasema tunataka kuita Kenya yetu “The Peoples Republic of Kenya” si the Republic of Kenya. Ni ya watu wenyewe.

Ya pili, tuliandika kuhusu Preamble, tukasema preamble ni ya maana sana.

Ya tatu tukaandika kuhusu mambo ya preamble na sitaki kusoma mtaenda kusoma.

Ingingine tumeandika principles of state policy na kwa mfano, so plenty political of _____, constitution, the law of the land lakini yote nimeandika kwa memorandum.

Jambo lingine ni kuhusu vile tunahitaji – kwanza tungetaka wale wazee wa mitaa walipwe pesa kama watu wengine kwa sababu hao wanafanya kazi ngumu sana. Hata wanafanya kazi ya amani na wanafanya pamoja na serikali. Kwa hivyo tumeweka hawa wazee wa mitaa wawe wakipata payslip yao kila mwenzi.

Jambo lingine ni kuhusu elimu – tunaona katika upande huu, au Kenya kwa jumla, tuko na committee mbili katika kila secondary school na hatutaka tunataka committee moja. Na hii committee moja inatokana na PTA. PTA sponsor, nini, tuchague kutoka wale na wafanye kazi kwa sababu watoto ni wao. Unaweza kutoa mtu ambaye hana mtoto kwa hiyo shule, hana interest kwa hiyo shule, kwa hivyo imbadilishwe. No Board of Governors.

Halafu jambo lingine nikuhusu masomo – tunataka free education kutoka pre-school mpaka university kwa sababu tunalipa korti mingi, tunauza vitu kidogo kidogo, tunanunua dukani, hiyo italipa watoto wetu.

Jambo lingine, tunahitaji 85% - 85 % inasaidia arid areas wale bado wako chini lakini tukisema tuje pamoja wengine wataumia.

Kwa hivyo 85% inatakiwa katika kila district. Na pia tunahitaji kila district wawe na shule moja ya National au mbili. Kama ile mashule ingine halafu wapate line kwa wale watoto wengine.

Na jambo lingine ni kuhusu mambo ya County Council – tunataka kusema wale ambao wanachaguliwa mayors, chairmen, wachaguliwe na watu wenyewe directly.

Halafu ingine, tunahitaji mambo ya siasa ingawa we have freedom of speech, tunaona ya kwamba vyama zimekuwa too much katika nchi. Kwa hivyo kama inawezekana, hata ninaona imepuguzwa, watu wana merge. They marry each other. Kwa hivyo inakuja chini, kwa maoni yetu kama ingekuwa nne hivi, ingekuwa mzuri. Ile strong strong halafu nchi inajengeka. Serikali ile ambayo tunataka ni serikali ya umoja, unitary government, ile kama vile iko sasa, President akiongoza, tuwe na Vice-President halafu kama ministers kama wale wengine.

Na jambo lingine ni kuhusu commissions – tunataka hawa kwa mfano cabinet ministers wachaguliwe au wafanyiwe proposal na bunge halafu iwe na commission ya kuchagua hawa; tuwe na commission mahali fulani kwa sababu wale wa juu watoe majina halafu na wanapeana commission halafu commission wanaangalia itakuwa namna gani.

Mambo wale ambao wanaenda bunge *interjection*

Com. P. M. Wambua: Joshua, maliza maliza tafadhali. Muda sasa umeisha nimekupatia overtime sasa dakika moja.

Joshua Kipkotor: Asante sana. Kwa hivyo tunaingia sasa habari ya utamaduni wetu. Utamaduni wetu ikae kama vile au religion ikae kama vile hakuna amendments. Hakuna amendment kwa hiyo, watu wenyewe wanafanya hiyo kazi. Ile mbaya wanatupa, ile mzuri wanafanya. Kwa hayo machache ninasema ni Asante sana.

Com. P. M. Wambua: Kuna swali kidogo, lakini kabla hawajauliza, kuna kitu ulitaja na sikuelewa vizuri, hii 85% ulisema ni ya nini?

Joshua: Ni ya watoto wa shule, wale wanateuliwa kuingia form one.

Com. P. M. Wambua: Okay, ngojea maswali, kuna mama anataka kukuuliza swali kidogo hapa halafu baadaye Commissioner Zein.

Com. Phoebe Asiyo: Mzee Joshua umeongea habari ya mashule, ile boards, na wewe unajua kwamba kuna sponsors wa shule bali bali, makanisa bali bali wanafanya sponsorship ya mashule zao, ungependa hii sponsorship iendelee au itupiliwe bali?

Joshua: Iendelee.

Com. Phoebe Asiyo: Iendelee. Na kama hakuna board, nani ataendesha shule, atasaidiana na walimu na wazazi kuendesha shule?

Joshua: Kuna Committee itachaguliwa kutoka na PTA badala ya board halafu inafanya hiyo kazi.

Com. Phoebe Asiyo: Swali yangu ya mwisho sasa – umetwambia kwamba maminsters yaani mawaziri, wachaguliwe na commission

Interjection:

Joshua: Kwanza proposal ni kutoka kwa bunge halafu wachaguliwe na commission.

Com. Phoebe Asiyo: Ningependa kukueleza kwamba kuna nchi zingine ambao wabunge hawachaguliwi ministers, wao wanajalilia mambo ya nchi tu, wanatengeneza policy na kadhalika, lakini ministers wanakuwa wale watu wa nje, wale ambao apana sio wanasiasa, bunge ndio inachagua hawa lakini apana wanasiasa. Unieleze kama ni hiyo ulitaka kusema au ulitaka kusema au ulitaka kusema watu hawa hawa wabunge ndio wajichague wenyewe minister au wachague watu wa nje wakuwe minister kama America inafanya, nchi ingine tena inafanya?

Joshua: Sitaki ya nje, mimi nataka wale tumechagua wachaguliwe ministers kutoka wale.

Com. Phoebe Asiyo: Okay

Com. Zein Abubakar: Mzee wangu swali nila ambatana na hilo ulirudishia mama mwisho, wewe unapendekeza kwamba bunge iteue watu watakao kuwa mawaziri halafu commission ichague katika wale walioteuliwa, lakini kulingana na miundo ya serikali, kazi inaofanywa na mawaziri ni kutekeleza _____ ya serikali kufuatia mwongozo wa kiongozi wa nchi hiyo. Ukiwa hutasema si kiongozi atakaye teua na kuchagua mawaziri wachaguliwe na bunge, huoni wabunge wanaweza kufuluga mwongozo wa kiongozi huyo? Kama ni kutaka kutilia maanani kwamba watu wanaochaguliwa kuwa mawaziri, wawe ni watu wanaofaa, wengine kama mama anavyokupa mfano, huwa wanampa kiongozi haki ya kuteua halafu bunge ikawahoji na kuwauliza maswali kuona kwamba ni kweli wanafaa kuwa mawaziri. Lakini ukisema ni wabunge watakuwa wanajibiga kwa nani? Kwa bunge, au kwa mtu ambaye anaongoza nchi hiyo?

Joshua: Nafikiri sikusema mkubwa wa nchi atupiliwe bali, nilifikiria, katika bunge yeye mwenyewe ako pale, if clear, ako pale pamoja na wale, so kwa hivyo kama vile umesema, ni mzuri yeye achague halafu wabunge wahithinishe.

Com. Zein Abubakar: Sawa.

Com. P. M. Wambua: Asante sana Joshua, asante. Jiandikishe hapo tafadhali. Tutamuita Joshua Mecha kutoka KNUT.

Naona hapo una maandishi, kwa hivyo lenga yale ya mhimu tufupishe maneno.

Joshua B. R. Mecha: My names are Jushua B. R. Mecha, I'm a peace member for Kabartonjo division the outstanding _____ chief.

In our union, we have written basing on the guidelines provided by the commission, if I just go through, because of time I know I will just highlight some few things since all what we have written is in this document.

First and foremost, we would like this constitution to have a preamble where this preamble should actually constitute *end of side A tape 1*

At least at any one time, this preamble should focus on the national philosophys and state manangement. Another issue, we look at the citizenship, the present citizenship is in order and we only like this kind of dual citizenship to be abolished.

Another factor is the President should only be responsible in terms of defence, national security and that he should be the sole person to declare may be war emergencies, national disasters, inse____, and breakdowns of public order that the President should have that power and nobody else to declare anything on security.

In the side of the armed forces, we should say that armed forces should observe the law of land outside the barracks that in some cases the armed forces when they come out, at times they become indisciplined and we want them to be guarded by the law so that when they are in the barracks they are disciplined in the barracks and arms of the barracks as any other member of the public.

Another issue is on political parties – we request that this nation should have only 3 main political parties and these parties should be funded by the government when it comes to election.

Another issue is that we adopt federal system and why do we say so? We said so because we say that some regions are well developed and some are not well developed and those existing resources in those regions should be guarded by the federal system of government.

On parliament we said that the parliament or the national assembly should be the sole body to visit higher posts in the government. For the case of may be the ambassadors, may be state personal states, commissioners, and any other so that when they are vetted they should be from the parliament. Proposals could be made in the house and those with good papers or those with papers relevant to those _____, we are going to say that they could now face the commission that will fade.

Another issue is the question of nominees of Members of Parliament should be scrapped but we are saying that special seats be preserved for the vulnerable groups like those disabled to handle that. May be the ladies *interjection*;

Com. P. M. Wambua: Please summarize bwana Joshua.

Joshua Mecha: Okay, I'm summarizing. We also said that the office of the President or the President should actually be the sole person who should be the Head of State, should also be the commander in chief of the armed forces, he should also be the Chancellor of state universities. We are saying this because if we appoint any other people, they may diffuse the powers of the President.

When it comes to election, we said that our President should have a direct election from wananchi.

Mayors and councillor chairmen should also be elected through direct voting. We are saying that for MPs and others, if one has to stand for election, if this person has been working in the government, we should not first of all retire because if we want to gather security, we are guarding that person so that next time if he is not going in, should go back and take his post in

whatever he has been doing.

The President should also attain a 25% votes in every federal region. Because we have written our memorandum I'm seing may be I have run short of time,

interjection

Com. P. M. Wambua: First you have exceeded by two minutes.

Joshua Mecha: So we feel that we have written our memorandum following the guidelines and we had written about 35 of them. So

Interjection:

Com. P. M. Wambua: Just for clarification Joshua, you are definitely recommending that the President be the Executive and it continues the way it is. Fine, Secondly, you have recommended that we have a federal system of government, and the reason you gave is that you want equitable distribution between the regions on resources, do you have anything to say? You definitely now there are some regions which are more developed than others, there are some which have really suffered under the present arrangement, are you recommending anything to equit that situation?

Joshua Mecha: In some cases, you will find that when it comes to things like education and ... okay, let me talk on the divisions because we are living at the divisions in the sense that in some regions they are underdeveloped. We find that there are some few schools and may be in terms of intake and other things, we are at a disadvantage because for a place to come up with may be a few schools, those schools should be guarded so that they distract %, somebody talked about 85% and we are saying that we recommend that system so that those who are in the disadvantaged areas, the few schools which are there should also be taken up by those from that region. We are seing that may be if that it traps any scrypt those people from the low lands or semi arid areas will be disadvantaged.

Com. P. M. Wambua: Okay, asante sana. Kuna swali? Ya, kuna swali lingine hapa ngojea.

Com. Phoebe Asiyu: Joshua umeongea juu ya dual citizenship, na unajua siku hizi na pia Katiba hii itakaa ata kwa miaka

hamsini, miaka mia moja, sijui wengine tutakuwa tumeenda, kama tulisema hatuwezi jambo hili, nataka unipatie hekima yako hapo, Kama kuna kijana wa Kenya ameenda kusoma America, akazaa huko, na mtoto akizaliwa America, saa ile yuko hospitali anapewa citizenship na passport yake pale kwa maternity, ya nchi hiyo, sasa huyu mtoto akirudi hapa na baba yake, tutafanya namna gani? Unataka mtoto huyu, atupe ile citizen ya kule alizaliwa, halafu apewe mpya ya Kenya au aje tu ile pia aweke tu kwa mfuko yake, lakini pia apewe ya Kenya, au tusahau yeye kule alizaliwa?

Joshua Mecha: Sisemi hiyo lakini vile ninaonea ni kwamba this dual citizenship ni kwamba wengine wanaweza kuwa registered may be in the process where may be that child is born but sometimes we have a problem, somebody could be a citizen of America, akirudi Kenya anakuwa citizen wa Kenya, mara anaenda nchi ingine anakuwa citizen, we have seen cases where may be some people register in more than 3 countries, and we will look at it and say, this people can cause a problem sometimes you cannot immediately say where this person comes from.

Com. Phoebe Asiyo: So can we say please in very special circumstances that this can be considered? Kuna kijana wa Kabartonjo ameenda ameo huko amerudi na mtoto yake kijana na ile barua ya huko, saa ile anapewa pale, ile sheria yao ni kupeana dani ya maternity.

Joshua Mecha: Why we refuse this dual citizenship ni mambo ya security, yaani mtu anaweza kuwa ... *interjection:*

Com. Phoebe Asiyo: Umesha fahamu, unafahamu?

Joshua Mecha: Yee, ni hiyo tu ndio tulikuwa naona otherwise, kama ni If it is in line to in ... interjection:

Com. Phoebe Asiyo: special cases?

Joshua Mecha: yaa, its okay but we only want to cut this question of somebody being registered here, registered there, and everywhere.

Com. P. M. Wambua: Asante sana Joshua, jiandikishe hapa. Tumeyapokea maoni yako na tuta tumwite Shem K.

Boiwa. Kwa hivyo tafadhali naona umebeba memorandum, summarize peke yake dakika tatu, tuwapatie wengine nafasi.

Naona watu wamezidi kuwa wengi hapa.

Shem Mbigwa: My names are Shem Mboigwa, I present the FFD that means Foundation for Dialogue incorporating with the CCR – Centre for Conflict Resolution Kenya.

Now I will just go very briefly, first of all I should say we should have a preamble in our constitution supremacy. The referendum should be conducted by the following:

Government Representatives, regions representatives and Non Governmental Organizations.

We go to political parties – We think that these political parties should be reduced to be if possible 3 in number. This is to reduce the division of the people in this country.

Structure of the government: This system of the government we wrote here I'm saying that we should have President as the head of state and then the Prime Minister and the head of the

Government and wish to retain the unitary system of government.

Legislature: Parliament should vet the following appointments, Attorney General, Chief Justice, and Auditor General, and Chairman of _____ all commission, they should be guarded by the parliament.

Now we say again here, those who are seeking for presidential seat should be above 40 years, parliamentary seat 30 years, and voters should be 18 years. Languages should be, those who require to seek for election in parliament, should be at least form four level and above. Likewise to local authorities, councillors should also be form 4 and above. And we said here, I think the illiterates have a right to recall their MP back if 75% of the voters in the constituency endorses. Because we have fear on some of the MPs disappear they don't come to their electorates, they come looking for votes, once they will be called they forget all about development in the constitution. So we feel the electorates have the right to recall him back. Likewise to councillors.

We also said their salaries should be in the _____ commission should be looked into determine their salaries. It should not be themselves who increase salaries for themselves.

Also we included here that we feel we should have two chambers in that house, that is the lower house and the upper house. A lower house is to have one member of the constituency ... *interjection*

Com. P. M. Wambua: Bwana Shem, I can see you are reading through the memorandum, three minutes are over, why don't you look at the head and summarize and then we will read the rest.

Shem Mboigwa: Okay, now we come to The chairmena and the mayor should be elected by the people. Also we said that this middle area we found a mineral in my land, we feel that if the government came and _____ on that land, the ownership be given 50% share in that area. And if he is evicted and he should be compensated fully.

The question of land property: In customary in our Kalenjini call it Tugen customary, we don't give lands to ladies, what we can give them is that come and cultivate and then they go. We don't give land to them. My recommendation is that we don't give land to girls we give only to boys,

Com. P. M. Wambua: And you want that to go to the constitution?

Shem Mboigwa: Yes we don't.

Com. P. M. Wambua: Is that the end of it?

Shem: Ya.

Com. P. M. Wambua: Thank you very much, ngoja,

Com. Phoebe Asiyo: Kama Mzee amezaa wasichana peke yake, hiyo shamba yake itakwenda wapi?

Shem Mboigwa: hataserve wasichana peke yake itapatikana.

Com. Phoebe Asiyo: kama msichana bado olewa?

Shem Mboigwa: Kama bado kuolewa? Pengine umnunulie plot aende akatoka customary hatukumbalii kuishi kwa ile shamba, pengine annue shamba mahali pengine.

Com. Pastor Ayonga: Kwa hivyo unasema, msichana ikiwa hakuolewa, atafukuzwa toka kwa boma ya mzee?

Shem Mboigwa: Apana fukuzwa.

Com. Pastor Ayonga: Ndio lakini kama yuko, na hebu ni kwambie, katika nchi yetu ya Kenya hii, sasa kuna wasichana wengi ambao hawajaolewa na wengi wamefikia kimo kile cha kusema sitaolewa, na yeye ni mtoto wako, anafanya kazi, anaishi boma yako, utamfanyaje?

Shem Mboigwa: Problem yake ni kwamba asizae watoto na kuleta kwa hiyo boma,

Com. Pastor Ayonga: Asizae?

Shem Mboigwa: Na kuleta kwa hiyo boma.

Com. Pastor Ayonga: Okay, kwa maana hiyo ni culture, ni utumaduni tutawacha namna hiyo, na hiyo ni maoni yako.

Shem Mboigwa: Maoni yangu ndio.

Com. Pastor Ayonga: Asante.

Com. P. M. Wambua: Ngoja kidogo, wee una maneno. (*laughter*)

Com. Zein Abubakar: Bwana Shem, you are suggesting that we should have a recall mechanism for Members of Parliament?

Shem Mboigwa: Ya.

Com. Zein Abubakar: You know the first Kenyan who is making such submissions to this commission, but everytime we ask people, you don't have to answer this question but if you feel you have something to say about it please do. How do you organize a recall mechanism? What procedure, what mechanism do you use? Secondly, how do you guard against abuse? Immediately after elections, those who were the opponents of that MP will start the recall mechanism. How do you implement the mechanism? Do you collect signatures? What do you do and secondly how do you guard against abuse?

Shem Mboigwa: Ya I think I state here we will collect signatures,

Com. Abubakar Zein: So you collect signatures 75% you said?

Shem: Yes.

Com. Abubakar Zein: and how do you guard against abuse?

Com. Wambua: Commissioners I want to know how do you guard against people forging signatures and saying 75% so toka?

Shem: We will appoint a chairman or somebody to come and _____ it.

Com. Wambua: Okay, we will accept that? Asante sana bwana Shem, just record your memorandum there and sign.

Councillor Alexander Mundani. Councillor najua kawaida maneno huwa ni mengi lakini leo yafupishwe. Lenga yale ya mhimu ya Katiba halafu dakika ni tano tu.

Councillor Alexander Mundani: Jina ni Alexaner Mundani. Ile jambo nataka kuzungumzia ni juu ya ma-case ya mashamba. Inaonekana ya kwamba, ma-case ya mashamba inakuwa nyingi na imepelekwa kortini mpaka high court. Ningeonelea ya kwamba, hiyo ma-case yote irudishwe kwa kijiji. Ipewe village elders, wazee ambaye wanajua waone ya kwamba hiyo case itamalizwa haraka iwezekanavyo.

Kuhusu soko huru: Ngingependelea kusema ya kwamba, soko huru imewekwa mahidi, kahawa, maziwa, na mimea mingine. Ngingependelea kusema ya kwamba, ile soko huru ambaye imewekwa, iondolewe kisheria halafu wakulima watafanya kazi kama vile hapo awali zamani. Na ile mahidi na vivaa vingine ambaye inatolewa nche kutoka America na sehemu zingine ifungwe ili wananchi wafaidike katika kazi yao ya mikono ya kulima. Kuna sehemu zingine nikirudia kusema ya kwamba, katika sehemu hii kuna sehemu tatu, sehemu ya nyada ya juu, kuna nyada ya katikati na kuna nyada ya chini na ukiangalia nyada ya juu imefanya development nyingi; serikali ilikata mashamba na ikapatia watu title deed lakini nyada ya katikati hakuna maendeleo yeyote ambaye imeyastawisha. Na nyada ya chini ya Soi, hakuna kazi ambayo inafanyiwa. Kwa hivyo tunataka kustawisha sehemu ya nyada ya katikati na nyada ya soi ile hata wale ambao wanaishi huko wafaidike.

Jambo lingine ni nasema mambo ya masingira: mambo ya masingira hapo awali, wananchi au wazee wa zamani walikuwa wakichunga misitu na kuifathi na kuangalia. Kwa hivyo tunataka wazee wapewe kazi hiyo na mkono ya serikali ipewe tu kidogo halafu hii mambo ya masingira ichungike vizuri sana. Kwa hayo machache asanteni.

Com. P. M. Wambua: Councillor asante sana, ulipendekeza kuwe na ustawi, sawa, katika sehemu hii ya Baringo ama Rift Valley. Unapendekeza iwe kila pahali kwa nchi ama ni hapa peke yake ambaye unazungumzia.

Councillor Alexander: Kila mahali katika nchi.

Com. P. M. Wambua: Kila mahali, asante sana councillor. Okay, jiandikishe hapa tafadhali. Okay kuna kitu commissioner angependa kutaja.

Com. Abubakar Zein: Councillor, langu si swali, mimi nimestaajabu sana kwamba huku misitu yenu bado iko sawa sawa, miti mnayo mizuri, kila mahali ukiangalia kijani, lakini bado una wasiwasi kwamba kuna watu wanakata miti huku?

Councillor Alexander: Sisemi ya kwamba watu wanakata miti lakini tunataka tu kuweka vikaso irudi kwa wazee, na serikali iko mkono yake.

Com. Abubakar Zein: Sawa mzee.

Com. P. M. Wambua: Asante sana councillor. William Chebet, William Chebet, mzee naona umejiandisha uko na memorandum, fupisha maneno ndio tuwaite wengine maanake watu wanaendelea kuongezeka tu.

William Chebet: *nenyune ko amache ng'alekab kindene Katiba ng'alekab kurithi.*

Translator: Yangu ni kwamba, nataka katika Katiba hii uridhi iwekwe dani.

William Chebet: *Eng' bitenyo achek ko kikochin murenik malik ko tebi tibik*

Translator: Katika mila yetu ya Kitugeni mali wa wazazi hulidhiwa na wavulana wafulana na wasichana hawalidhi.

William Chebet: *Ngunon komite lagok chemaitun chi ko kimoche kenai ole tononen.*

Translator: Na kwa sasa kuna wasichana ambao hawajaolewa na tunataka Katiba itangaze msimamo wa kuwalida hao.

William Chebet: *Kogeny ko mito mogoriot ne masiku werik*

Translator: Pia kuna pachiri ambaye hajabarikiwa kuzaa wavulana

William Chebet: *ko nguno kotinye tibik ko mie koib malicho e.*

Translator: na kwa sasa kama yeye amezaa wasichana, ni heri wasichana walidhi mali ya mzazi huyo.

William Chebet: *Mi lagoi alake che motinye kwanisiek che menget kwanisiek,*

Translator: Kuna watoto wengine ambao wazazi wao hawasaidii, wazazi wa kiume hawajulikani wako wapi.

William Chebet: *kimoche kindene Katiba konyor ole motun ko tebe.*

Translator: Tunataka wao wawekwe kwa Katiba yajulikane msimamo watasimama na watakuwa namna gani.

William Chebet: Ni hayo tu. Asante.

Com. P. Wambua: Asante sana William Chebet, jiandikishe hapa tafadhali. Maneno yako ni masafi, ni mazuri. Kabla hatujaendelea ningelipenda kumtambua mwenyekiti wa Kanu Baringo district ambaye pia alikuwa hapo awali MP wa eneo ili Bwana William Kamuren. Karibu mheshimiwa. Tutakupatia nafasi najua uko na mengi ya kusema lakini kwanza tuwasikize watu wako halafu tutakupatia ukiwa tayari. Wawili watatu tutakupa nafasi. Kwa hivyo tutamwita Ezekiel K. Chemelil. Naona hapa umesema utatupatia written memorandum kwa hivyo maneno yafupishwe. Lenga tu ile ya muhimu kwa summary halafu basi.

Ezekiel K. Chemelil: Nitajaribu. Majina yangu naitwa Ezekiel Chemelil. I will go straight to the point. Nitaanza kwa those candidates seeking for presidential seat. Qualification should be a degree and above.

Should be somebody mature enough, experienced in politics more than 10 years or if he was a civil servant he should have served as a civil servant more than 10 years.

Kwa upande wa Bunge or Civic Local Cabinet: councillors na wabunge – Katiba hii tunaitengeneza, unajua ili Katiba ilianza mwaka wa 1963 mpaka sasa. Hiyo Katiba was fit for those years up to now lakini Katiba tunayoitengeneza sasa ili itachukua miaka mingine zaidi ya arubaine. Kwa hivyo, at that time, lazima tuangalie sawasawa na kwa hivyo maoni yangu should be a

form 4 or equivalent. Mbunge ama councillor.

And then he should be tested in English and Kiswahili.

Mambo mengine ni kuhusu mambo ya land: mambo ya land kuna some communities whose land was taken for public utilities may be to build schools or markets or hospitals and they have not been compensated although the commissions have looked into. Tunataka hiyo iingie kwa Katiba ya kwamba kama kuna mambo namna hiyo watu walipwe kwa sababu some of the communities have been left landless and they had land.

Kitu kingine, msichana nipozungumzia Mrs Asiyo, hebu nikuje kwa macho ine Bwana mkubwa yule alitusimamia jana, amesomesha msichana yake, ameenda America, anaporudi kufanya kazi Nairobi anakuta kijana anakunywa pombe na hatafikani kukunywa pombe na hatafikani akunywe pombe, ako na degree, unasikia ameo huko, haifiki kwa wazazi. Baba ya yule msichana anagoja apatiwe msaada ama ni haki kwa vile alimsomesha. Wengine ni wakora wanakuja wanasema, “wee Mzee wacha”. Sheria inasema kama ushaua msichana ushaua hata kama ako na degree umeoa, ameenda. Sasa yule mzazi na hata nyumba yake inabomoka, kwa sababu tena ameenda kwa taabu huko anapotea. Kama aliolewa Mombasa kwa

mheshimiwa commissioner kijana huyu, na msichana ni mkalejini anaenda anaonewa anaonewa, ulitoka wapi, ulitoka mbala, unaonewa, unaweza kutobolewa hata macho. Msichana vile vile kutoka kwa meru akiolewa hapa Baringo, anaweza kuolewa na mtu mlevi ama ni mtu fulani kama mimi, hujui kama niko na elimu category gani, nimeoa msichana, si mi ni bwana? Mtafanya nini? Nashorota sheria ya mtoto ya mwenyewe ingawa hata Mungu hakubali. Waheshimiwas, Wanacommissioners, mutuundie sheria ya kuchunga watu kama hawa ndio mwenye aliyemzaa msichana afaidike.

Kitu kingine msichana wacommissioner, macho ine huyu kijana, bwana anasema wewe ni kijana saa hii lakini katili. Msichana wako anasoma hapa kabartonjo, kijana yangu anadanganya hapa hivi hivi, labda alikosa school fees, unasikia amepata mimba, alikuwa form 4, wewe huko unasema, “Ah si amepata Mtugeni, Mkalejini, iko nini, na mimi siwezi kubali kijana aingie kwa mboma yangu, nakomboa nyumba hapa anatangatanga, na wewe umepotesha pesa mingi. Sheria iundwe ya kuchunga wasichana wetu wasiolewe hovy hovy na isitumiwe hovy hovy.

Ingingine ni ya kwamba, mnapotwambia katika Kenya ni mbunge. Mbunge tunaamini aende akaunde sheria ama apitisha yale tumepitisha kwa bunge inakuwa sheria. Wabunge sisemi mbunge hapa maana nikisema mbunge mtu atasema ametaja mbunge wetu, hapana, bunge yote, tunajua Kenya tuko na wabunge mia mbili na kitu. Mbunge kwenda huko alikuwa anakula elfu mia moja ishirini na marupurupu. Kuingia huko tunasikia mshahara yake ni elfu mia sita, elfu mia saba. Na sisi hapa watoto wanaomba ile kitu inaitwa bursery. Watoto wa masikini wakiomba bursery, hakuna mtu anakibisha bursery mpaka Nairobi, councillor anakula hii pesa rupurupu kidogo kidogo, inaishia Naivasha, na ako na karatasi ine za wale watu ambao wanaomba bursery. Yule mbunge anakula bursery yote anamalizia Nairobi naye huyu councillor hafiki Nairobi, na hata akifika Nairobi anapata lodging ni kutoka mia mbili mia tano, hana kitu. Kwa hivyo tuundie sheria ambayo inaweza leta hiyo bursery isimamiwe na village elders ama kamati fulani katika division ama district. Ikiwa chairman ni chief ama sub chief ama DO kwa division hiyo, itaenda vizuri.

Kitu ingine ningomba ni katika Kenya mnatuambia leo niko, mnatuambia tumeomba msaada ng'ambo ya projects, Baringo million tana inaweza kuingia, nikisema Baringo sina _____. Baringo inaweza kuingia million tana na inaishia kwenye hawa watu wenye matumbo hapa watano. Na mtu anapelekea bibi yake anaweka kwa mattress halafu anatoa moja

moja anatisha nayo watu wengine. Kama alikuwa anang'ang'ana shamba na mwingine, anaenda anatafuta lawyer. Si wewe unapotea, unalala nje. Mimi na tena Kenya inasema imesolotika kwa sababu gani na pesa ilikuja? Mimi ningependelea kuwe na marekebisho kwa hizo pesa. Maana anayeua matunda Kabartonjo apatiwe elfu tano, kama inawezekana apatiwe elfu kumi, mwingine huko na huko ndio wawezeshe kusaliza hiyo pesa kwa sababu hiyo pesa itaingia kwa city council itaweza kuingia kwa serikali maana inaingia kwa kulipa _____. Na tena utajiri kidogo kidogo unaanza kulekebisha lakini hizo pesa zetu za Kenya zimeishia kwa watu wawili hiyo ndio madhala.

Kitu kingine,

Interjection

Com. Abubakar Zein: Ya mwisho mzee wangu

Senyenge: Kitu kingie commissioner

Com. Abubakar Zein: Ya mwisho mzee wangu

Senyenge: Asante sana. Kitu kingine ya mwisho ninamaliza tu kwa sababu bando ninatuma hiyo memorandum yangu.

Kitu kingine ya mwisho ni ya kwamba mimi ninapona katika watoto wa shule, mashule hizi tuko nayo – shule za Primary nimetembelea sehemu zingine, shule kama Kabartoj primary iko na secondary katika sehemu zingine. Tungekumbaliwa muongezwe muda wa kuunda sheria na msaidie upande wa education maprimaries zote katika Kenya waweze kufungua masecondary schools. Tusigojee kusema ati hamjamaliza kutengeneza hii sheria, na hii, na mashule hii kubwa kubwa kama Kapropita na mashule zingine kama Mang'u ziwe National watoto wetu wachanganyike kwa sababu tumeona hiyo mashule zinasomewa na kabila moja, watoto hawawezi kuwa na akiri. Na hiyo mambo ya 80% iendelee. Asante sana commissioner. Sina mengi.

Com. Abubakar Zein: Asante sana mzee asante sana. Tafadhali ukimaliza kuandika memorandum, iwe kabla ya mwisho wa mwezi huu kwa sababu ikifika mwisho wa mwezi huu nafikiri tutafunga kupokea memorandum, tutakua tumemaliza mkoa wa magharibi mkoa wa mwisho. Tutakuwa tumeanza kuandika report. Kwa hivyo utume kabla ya mwisho wa mwezi huu lakini kwa sasa jiandikishe pale jina tafadhali.

Senyenge: Asante sana, nitakibisha hii memorandum yangu.

Com. Abubakar Zein: Sasa, kwa niaba ya Mwenyekiti ningependa kumuomba Bwana Samson Chemoitich, Samson, Kama Samson hayuko karibu, kiasi anaitwa Job Chesaro. Mwanasiasa Karibu bwana. (*laughter*) karibu sana, tulikuwa na yeye jana huko akinionyesha hizi mipaka ilivyo kati ya hapa na Baringo.

Job Chesano: Asante Bwana commissioner. Langu ni mengi lakini kwa sababu ya dakika tano haiwezi kuniruhusu nisome zote lakini ningeomba tu nitaje kuhusu ardhi. Ardhi ya nchi hii haikuangaliwa vizuri katika Katiba ilie iko saa huu. Sasa ningeomba commissioners Katiba hii inaingia sasa ionekane vizuri kama hii sehemu ya forest. Hii sehemu ya forest ilikuwa shamba za wenyewe na wazungu walivyo fukuza hawa, wenye shamba hili hawakupewa compensation. Sasa Katiba hii inatajikana ionekane wazi wazi ya kwamba hawa watu wenye walifukuzwa haki yao iko pande gani.

Katiba ya pili tunataka kuonekana katika madini ile iko nchi hii wenye sehemu hiyo wafaindike na hii jambo la 75% iwe mwenye alikuwa na own hiyo land. Kwa sababu tunaona hata sehemu za nyada za chini zile zinaonekana mahali ya mafuta, _____ aina bali, bali. Kitabo ile ikipatikana _____ mambo mengi dani ya hiyo ardhi, hakuna mtu, county council wanakimbia straight wanasema hapa ni sehemu ya serikali. Kwa nini Katiba isionekane wazi wazi ya kwamba mwenye ardhi hiyo afaidike kwa sababu hata Mungu naye amempatia hiyo mamlaka iwe yake.

Kwa kukamiliza kwa sababu hii ni sehemu mrefu sana, ningeonelea kwa memorandum yangu ya kwamba, kama sisi wakenya tuangalie kuhusu vijana wetu kutoka watoto kutoka

Upande wa elimu: Elimu ionekane wazi wazi ya kwamba iwekwe sehemu ya kusomeshwa kutoka pre-school mpaka class 8 at least iwe free education na pia hata form fours. Iangaliwe sana sana kwa sababu economy ya nchi inaongozwa na elimu. Kwa sababu sehemu ambayo haina elimu haina nguvu. Bwana commissioner, finally kwa sehemu ya memorandum yangu mimi ningeonelea ya kwamba hii mambo inaitwa ya majimbo. Selikali hii iwe serikali ya majimbo. Federal government. Na hii

majimbo inamaanisha kila mtu atatabulika mahali atapokuwa ko. Ninaweza kuwapatia memorandum wanacommissioners, sina mengi kwa sababu nikisema yote itachukua muda na mi nasema asante Kwa si kusema jina saa ile, jina langu ni Job Chesaro naakirisha network ya _____ Association, Po.Box 729 Kabartonjo Thank you very much.

Com. P. M. Wambua: Asante sana Bwana Chesaro, jiandikishe huko tena. Kuna mama ambaye angelitaka kuzungumza, kuna mzee alikuwa na mzee alikuwa ametajwa? Samson basi endelea hapo.

SamsonChemwetich: *Ane kegurenon Samson Chemwetich.*

Translator: Mimi ninaitwa Samson Chemoitich.

SamsonChemoitich: *Ko anyun tuguk che amache ateb ko ng'alek somok.*

Translator: Mambo ambayo ninataka kuuliza ni mambo matatu.

SamsonChemoitich: *Che bo tai ko somanet.*

Translator: Jambo la kwanza ni elimu,

SamsonChemoitich: *Togu somanet ko woin sait age.*

Translator: Naonavyo masomo huenda wakati mwingine hapa unaonekana hauendelei vizuri.

SamsonChemoitich: *Amun mito somanet ne somani chito ago kiruchi kwandanyi timdo anan ko kikoalda tuguk chemi kaita kobek ak ye kaiyakonam somanet ko kwo timin koam ak korket en olio.*

Translator: Kuna elimu ambayo mtu hupata baada ya mzazi yake kupambana kabisa juu chini baada ya yeye kuelimika na kupata mapato, anapotea.

SamsonChemoitich: *Koyaga anyun korshe chon koyam tutu ak koam keser*

Translator: Na yule mzazi anapata kuwa na giggers pamoja hata na chawa.

SamsonChemoitich: *agot kwiyo ko matyeche, tyeche ng'wony ako kisoman lakwenyin.*

Translator: Hata viatu hana anakanyanga ardhi bure na mtoto yake amesoma.

SamsonChemoitich: *Ko agenge noo.*

Translator: Hiyo ndio jambo la kwanza.

Com. P. M. Wambua: Proposal, proposal, Pendekeza ni nini hapo. Ungelipenda tufanye aje?

SamsonChemoitich: *Ko non ko amache anyun ketoben kele yon kele ara ngo tesu banan somanet.*

Translator: Hiyo anasema inaonekana hata elimu huenda unachangia kwa upande mwingine umasikini.

SamsonChemoitich: *Amache keng'at ng'atutiet ne kimoche chin ne kisoman kwan agot agine kayaton che bo kasit ne kiyai. Chi ne kisoman ko mechei koam sigik agot agichek chebo kasit ne kiai kosomesani bichu.*

Translator: Kwa elimu mtu akishaelemishwa vizuri na wazazi wake anapatwa kuwapa wazazi sehem ili hata na wao wapate kufurahia matunda ya elimu ya mtoto huyo.

SamsonChemoitich: *Amun ki bitetab tugun en achek ko cham keenye tuga anan ko nego ko mite banyek ab boonde, kelenen banyekab boonde chu.*

Translator: Katika mila yatu ya tugeni, wakati ng'ombe anachijwa, kuna sehemu ya nyama ya mzee ambayo lazima mzee apate.

SamsonChemoitich: *Ko u non chebo Chepyoset, tinye kora chepyoset che chik, chebo chebo chepyosoi. Amache anyun konyor bichon banyekwak chebo mushahara, kimoche konyoru mushahara agot inye chebo kasarta nyin.*

Translator: Hata hivyo hivyo hata kwa mama kuna sehemu za nyama ya ngombe ya mama kwa sababu inasemwa hivo. Basi kama hivyo, tunataka mama na baba wapate sehemu yao ya nyama yaani kwa elimu mapato ya mtoto wao.

SamsonChemoitich: *Nebo aeng' anyun ko ni, mi ng'olyon age ne aroti, mi makosa che yaei alak kerat*

Translator: Jambo la pili ni hili, Kuna makosa watu wengine wakifanya wanawekwa korokoroni.

SamsonChemoitich: *Korok kenam kebokeratchi district age ne mo emenyin.*

Translator: Na wanawenda kuwewa korokoroni kwa district ingine ambayo si kwao.

SamsonChemoitich: *Ko makararan iman, moche keng'alalen kio, amune si komokirotyi bik district ne ng'wai?*

Translator: Naonavyo si jambo jema kwa sababu gani hao wasiwewe kwa jera kwa district yao.

SamsonChemoitich: *Motinye ole kirotyin anan motinye tuguk che kiyoi?*

Translator: Kwa hiyo district hawana mahali pa kuwewa kwa jera au hakun akazi ya kufanya katika district hiyo.

SamsonChemoitich: *amache ye kirat bik kerotchi district ne ng'wai.*

Translator: Watu wakifungwa wakishafanya makosa wafungwe kwa district yao.

Com. P. M. Wambua: Umemaliza?

SamsonChemoitich: *Oret age ko nebo kumik.*

Translator: Jambo lingine ni pombe,

SamsonChemoitich: *Emoninyon ko komen kitor gie ng'o.*

Translator: Kwa inchi hii yetu, pombe ilikuwa na kazi fulani.

SamsonChemoitich: *Ko kibo maana, kibo tumwotin.*

Translator: Pombe ilikuwa inatumika kwa wakati wa serehe za utamaduni.

SamsonChemoitich: *Ko kibo tumwotin ago kimakichamchin chepyosok che tagomengechen ak murenik che mengechen.*

Translator: Kwa sababu katika kitamaduni, haikuwa inaruhusiwa akina mama ambao ni wachanga na watoto wanyue pombe.

SamsonChemoitich: *Amun bichon kokirkyini bik, che ribe lagok chepyosok ko murenchu ko ribe emet en bunik anan ko tyong'ik.*

Translator: Kwa sababu wakina mama ni wachungaji wa watoto na wanume ndio wanalinda nchi.

Com. P. M. Wambua: Can you please encourage him to give us proposals in respect of those issues which he think are problems so that we can give somebody else an opportunity.

SamsonChemoitich: *Ko raini anyun ko kokomelmoo komechon kikuren tugul bo boisioi ko kiyakitun en bik che mengechen. Kora anyun ko amache keyai kele en bichon bo che kisomesoneko mwisho konyor kebebertanyin. Wektoi komen emoni kowo let. Kolyan makibir marufuku bichon yachen?*

Translator: Kwa sababu pombe basi imeenda kuharibu watu katika nchi, constitution ipige marufuku unywaji wa pombe.

SamsonChemoitich: *Hasa chu yachen chu bo kartasi ko chekatar agot lagok cheb sugul.*

Translator: Hata zaidi hizi ziko kwa karatasi zimemaharibu watoto wa shule

SamsonChemoitich: *Ko amune si kochamchin serkali bichon licence bichon?*

Translator: Asema, Bona serkali inapeana licence kwa hao ambao wanatumia vitu kama vivyo kuharibu watu wetu?

Com. P. M. Wambua: Ambia mzee, tumesikia mzee kwamba unataka kwamba pombe ipigwe marufuku. Tumeandika tayari.

SamsonChemoitich: *Mamiten ng'olyon age, nga'lekyuk chon.*

Translator: Hakuna jambo lingine ni hayo tu.

Com . P. M. Wambua: Sawa.

Asante sana, jilandikishe huko tafadhali. Nasikia kuna mzee mwingine hapa ambae ako umri. Ako wapi? Anaitwa Musa Samukwo. Na kweli ni mzee. Tumekupa nafasi hiyo mzee lakini maneno yafupishwe ndio tumwite mwingine. Na kuna mama mwingine hapa ambaye tutamwita baada ya mzee kuzungumza, Lina Chesoni Mrs. Yuko? Tutakupa na nafasi mama baada ya mzee Samukwo kuzungumza halafu atafuatiwa na Peter Kiboweni. Akae chojo. Keti mzee kama unataka. Wacha unasimama vile unataka au unakaa chini.

Samson Samukwo: Bwana mwenyekiti Bwana commissioner, nakuomba uchunge saa kwa sababu mimi kweli sikusoma vizuri. Nasoma kidogo tu lakini mimi naona watu wanaingiza hapa maendeleo sijui hii sasa ni kuweka sheria au ni maendeleo? Hapo ndio mimi naona wengine wanaingiza maendeleo lakini mimi nafikiri kwa maoni yangu nikutunga sheria. Basi wanacommissioner, nyinyi wote wazee na wamama hamjambo? Bona mnanyamaza? Hamjui jambo ni ya Mungu.

Basi Bwana Commissioner, maoni yangu: mimi nataka hii siku, hii miaka imewekwa kwa sheria ya kwamba Rais anakaa miaka tano na kama anaongeza ni miaka ingine tano halafu inatosha. Mimi nataka ifunjwe kwa sababu tunaweza kutupa mtu wa maana sana. Unaona wakati wa Kenyatta, Kenyatta alishika nchi hii Miaka kumi na tana, pengine kama ingekuwa miaka tano, miaka tano, pengine mwingine angetuangusha sisi. Sasa tukipata mtu wa maana, bora kura tu inaamua. Sasa mimi nataka ifunjwe.

Ya pili, mambo ya majimbo: mimi nataka sherikali ya majimbo kwa sababu kuna majimbo ingine inafurugafuruga watu na kuna majimbo ingine watu wanakulia. Kwa hivyo serikali ya majimbo mimi naona ni mzuri lakini si kutenga watu. Kama watu wako sasa majimbo kama Rift Valley, kama kabila yote iko Rift Valley, naheshimu na mali yake, hakuna kusema ati inafukuza, bora yeye anaimba nyimbo ya hiyo province. Sio mtu kukaa na mali yake.

Ya tatu, mimi nataka serikali iheshimu mtu na mali yake. Kama inatakiwa shamba fulani au kitu fulani, isiulize mtu kwa nguvu na

kama mtu anataka kitu fulani anapatiwa kitu fulani. Si kuchukua bure.

Ya nne, mimi nataka sheria ipitishwe kimila, hata sasa vile nazungumza sasa. Mimi nataka Katiba ya Muafrika, sitaki Katiba ya mzungu. Mimi nataka mtu akiwa na bibi wake wawili, au watatu, afunge ndoa yote, kwa sababu ikifungwa ndoa moja na wale wengine wanakaa tu bure, wakati yule mtu anaenda, hao wengine wanaweza kunyanyashwa.

Ingingine ya tano, kwa mila yetu watoto ni wa mwanaume sio wa mwanamke. Hata ukiona kwa Bibilia jina ya watoto ni ya mwanaume. Kwa hivyo watoto ni wa mwanaume.

Mimi nakuja tena kwa upande ya hii mambo mnasema usawa. Kweli elimu ya msichana na mvulana ni sawa. Kazi ni sawa, lakini usawa ya uongozi, siwezi kukubaliana ati mwanaume na mwanamke ni sawa. Mimi nakataa kwa sababu mila yetu, kufika jioni, mwanamke anatandika kitanda sio mwanaume anatandika kitanda na mwanaume haendi jikoni. Wacha hii maneno ya wazungu. Sisi kweli ata kama tukiishi kama bibi ni P.C. jioni anatandika kitanda na anaenda jikoni. Wanaume apana enda jikoni.

Mimi nasema nakuja tena kwa kijana na msichana. Kijana kwa sisi mila yetu, huwezi kugawanyia shamba kijana na kugawanyia shamba hata msichana, halafu kijana anazaa halafu msichana anazaa. Sisi kwa mila yetu tunasema hapana. Hawa watoto wa msichana ni hata damu sasa itapotea kwa sababu huyu msichana analeta damu ya kila mahali halafu na haleti shamba. Sasa huyu kijana kwa shamba, hiyo mbegu yake itakuja kunyanyashwa na hawa. Kwa hivyo mimi nakataa lakini kwa kupatia msichana yangu ng'ombe, kwa kupatia pesa, ama kitu fulani aende asikae nyumbani. Hiyo ni mila yetu.

Com. P. M. Wambua: Imemalizika? Umemaliza mzee? Eh.

Samson Samukwo: Sasa, nimemaliza.

Com. P.M. wambua: Asante sana kwa maoni yako hayo mema, tafadhali jiandikishe hapo halafu Mama Lina, tafadhali

taja jina na utupatie maoni yako.

Lina Chebun: Kwa majina mimi ni Mrs. Lina Kibuni. I have come here to present personal feedlings or observations. Nimeonelea ya kwamba watoto ni wa kila mtu, thus says the parents. The parents are responsible for any child's welfare but today we find that most of the responsibilities are left to the mothers. So there should be a constitution that whoever will not have taken the responsibility, if you are a man or the father, then steps should be taken.

Another thing is that you find that in the constitution, the MPs in parliament are the ones who discuss on what they are supposed to get. That should be left to a body. A body should be set so that they discuss on any other _____ use because if that is to be allowed, then every working sector should be given that right to discuss on their own salaries. So a body should be set to discuss the salaries of the MPs. I also feel that the councillors who are very much near to the people are given too little and yet they are the ones who work more than the MPs. You find that an MP goes even for 2 years without knowing what is going on in his constituency. So it should be backed that as people have said, they should stay for at least may be 2 (I'm talking of the MPs now) they should be visiting their people regularly. They should not be given even two years. They should go for an allowance of one year and if they don't come back to the people, then the people are empowered to recall him and may be pass a vote of no confidence. Also an MP who moves from one party to the other should seek the mandate from his people that is from those people who voted for him. So a constitution should be set so that nobody should be shifting from one party to another.

On nomination, I will say nomination be there but because ladies are people who (may be I turn them as may be cowards) they don't like to express their feelings. They should be given the chances when nomination comes if there will be but I feel nominations should be there and should be looked at on gender issues. Again we know ladies may be looked down by men when they are contesting, so when they are nominated they are just silenced especially following the culture. We have come here and I have also very many people talking of the culture and if you look at it, the ladies will shy off that is if they follow the culture. So when nomination will be allowed, then I wish the ladies could be considered.

I want to go back to the MPs. We find that in our secondary schools there are so many children who are unable to pay school

fees and the schools suffer so much because of the balances. The MPs in every constituency should be given the responsibility of those who are unable because of the poor conditions of those areas, they should be given that responsibility so that they just be going there to check whether there is anybody who is suffering so much because in a school you find a child having may be a balance of over 100,000/- and the parent has not been able to pay that. You find that the MPs when they go to the parliament they say that children should not be chased. So I want a constitution to be set so that the MPs are given that responsibility of this balances in schools so that they give burseries to those schools which they find there are so many children who are unable to pay fees.

There is also the mandate, because there is this national maendeleo, may be it is not supposed to be there in the constitution but I want to add that a constitution be set so that those who elected ladies who have been elected on the line of maendeleo should also be coming back. They are almost like the MPs, so they should be coming back to the people who voted them in to hear their views and also their feelings and may be to look at their welfare also because there may be a _____ or even ... let me have a project which was started by the ladies but you find that the top ladies are the ones who are benefiting leaving those ones on the crowd. Up to there that is.

Com. P. M. Wambua: You have finished? Okay, thank you very much Lina. Please register yourself there. Ningelipenda kumtambua Bwana Ezekiel Komen ambaye alikuwa hapo awali Managing Director Kenya Pipeline. Bwana Komen ukiwa tayari utujulishe tutakupatia na nafasi ya kutoa maoni yako. Kwa hivyo kwanza pengine uwasikize wananchi kidogo. Utataja jina Bwana Komen, inaswe kwa machine halafu utupatie maoni kwa kifupi.

Ezekiel Komen: Asante sana Mheshimiwa, commissioners ambao wako hapa, hata mwenyekiti ako hapa wakati huu na viongozi wote Bwana DO na viongozi wa talaka bali bali. Mimi Bwana Mwenyekiti naitwa Ezekiel Komen, natoka sehemu hii, huku nyumbani naitwa Lokoloti Bosi na mimi ni mzaliwa wa hii location Kerio, constituency ya North Baringo. Kweli umesema na ni juzi nimestaff kwa kazi baada ya kutimisa ile miaka inatakiwa na ninashukuru Mungu sana kwa kunifikisha hapo na kushukuru pia sherikali for providing and enabling environment kutoka wakati nilianza shule mpaka wakati huo wote nilifanya kazi, na kushukuru tena mtukufu Rais maana katika kazi ya maofisi ya mwisho ambao nilitimisha kwa miaka karibu nane, ni kwa

ajiri ya appointment yake.

Basi bila kupoteza wakati kwa sababu nafasi ni ya watu wote, naenda kwa kuwasalimia wananchi wote, hamjambo? Asante sana. Hii ni kikao cha heshima sana na hii ni sababu nimetoka Nairobi Bwana Mwenyekiti kwa kuheshimu kazi yenu.

Kwanza nilipojitabulisha nilisema mahali natoka na kwa ratiba hiyo, ningependelea pengine sitasema kwa Kingereza zaidi kwa sababu nikisema pengine maana ninatoa maoni ambayo inawakilisha maoni ya hao watu na ningetaka pia wawe informed wajue ninasema nini. Ningependelea Bwana Mwenyekiti hiyo Katiba ya Political ama boundaries ya kawaida kutoka sublocation, location, district, mkoa, na sisi kwa Kenya iheshimiwe. Isiwekwe na wakati wowote wa kusema nchi imekuwa free hakuna boundaries. Na ili sisi tujue ya kwamba tunatoka sehemu fulani na tukiuheshimu hiyo mpaka juu kule tukiwa watu wa Kenya na inaenda kama East Africa na African na ulimwengu ambao sisi ni jamii moja. Napenda hiyo ifuatiwe. Na kwa hali ya kugawanya sehemu hizo iendelee Bwana Mwenyekiti kulingana na diversity, kulingana na population, kulingana na watu, watu wakiongezeka, location ya Kerio igawanywe, District igawanywe kulingana ili ipatane na mahitaji ya wananchi ili pia serikali iwe karibu na watu. Hiyo iwe dynamic, iwe ikiendelea, isikome iendelee mpaka maana tuna watu na kuzaliwa kwa watu, mambo ya family planning iko lakini sikusema watu wasiendelee kuzaa. Sisi tunaamini watu lazima wazae wajaze dunia maana hili ni Mungu alitupa, kwa hivyo watu wanapoongezeka igawanywe, igawanye, bora tu watu wanapanga kulingana na uwezo wao.

Jambo lingine Bwana Mwenyekiti ni uongozi. Katika hali ya uongozi, uongozi ianzwe katika village; kuwe na elders ambao wanachaguliwa na assistant chief wa sublocation, location chief awe na location na team yake pia. Sublocational team ya wazee, ya elders, si wazee peke yao, representatives ya wazee, youth, na watu wa kanisa, na watu wa taraka bali bali ili watatue maneno ambayo inakuja. Kwa nyumbani na kuelekea huko mbele ili kesi isipelekwe tu kortini kila wakati, kufunga watu maana watu wanatumia hali ya kisirani tu kupeleka hata mtu ambaye anajua. Nikipeleka nakufanya maneuvering mtu anafungwa bure kwa sababu ya uwezo ya.... Lakini waze wanajua hii inakaa namna hii, desturi ni hii, na wanafunga, iko maneno ya kufunga watu. Iko njia yetu ya kufunga na mtu akifungwa na wazee ama elders hiyo ni kali kuliko hata ile ya kortini maana unakuwa identified right from home na utajulikana. Pahali halitasikia iendelee kwa viongozi iwekwe chief, iwekwe assistant chief, iwekwe DO, mpaka DC, mpaka huko juu, PC. Hatuwezi kukaa, watu wetu wamezoea hiyo, wamezoea hiyo

routine ya kuwa na viongozi wa kutawala watu. Maana ukiambiwa tutapeleka wewe kwa chief, mtu anaanza kusilahi didogo, ananza kuogopa na watu wanaanza kutunza sherias. Lakini kama hakuna chief, hakuna DO, hakuna DC, dunia itakuwa mbaya.

Kwa hivyo hali ya utawala iwekwe. Right up to home. Ni kama hata kwa mama, kwa boma, mzee wa mboma ni mzee wa mboma, mama ni mama wa mboma. Wakati mzee hayuko, mama ndiye anaongoza mambo yote na kadhalika. Kwa hivyo hiyo uongozi iwekwe na hiyo mimi naung mkono kabisa.

Jambo lingine ni hali ya kuchagua hawa watu, hawa viongozi. Viongozi wa location, sublocation, mimi nataka irudiwe ile ratiba ya zamani ya mlolongo kusema huyu ni kiongozi wetu. Assistant chief ni hiyo tu. Mambo ya DO na DC hiyo serikali iangalie ni sawa lakini ile local ni very effective, ichaguliwe na wananchi. Line mrefu, kama hakuna line, basi unarudi nyumbani hapana kuwa chief, utakuwa chief wa nani na we hauna mtu ambaye anakuamini maana watu wetu wanajua ni nani anaweza kuongoza vizuri. Wanajua kulingana na tabia yake. Wanajua tena kulingana na ukuu, watu wa fulani fulani wamekuwa wakituzia inchi, watu fulani wakichuna inchi, inchi inabalikiwa. Kuna watu wengine, s(isemi walioko ama nini,) lakini wakiongoza inchi inakuwa na mafurugano. Kwa hivyo those ones should give way, its not allowed, waforce watu na kudictate, hapana. Kuna hii vitu inaenda na baraka ya watu. Hiyo uongozi tena ipewe hata akina mama. These days hata akina mama wamekuwa educated, kwa hivyo, hata kama ni assistant chief, crown mama anapewa kama anauwezo. Bora tu aende kwa line na wazee wabadirishe ile mwenendo ya kusema “mimi apana enda kusimama nyuma ya mama”. Lazima kama yeye anaongoza na ichi imbalikiwe, basi, unataka nini ingine? Na hivyo hiyo mpaka location iwe viongozi kama hiyo. Hii utawala tena Bwana Mwenyekiti ningetaka kutanja ya kwamba, utawala ya inchi pia iende kulingana na uchaguzi. Location sawa, na kila location iwe na uchaguzi, kila location iwe na councillor na wawe councillors wenye kuform ile council ya district. Wenye kuchunga rasimali ya nchi, boundaries ya nchi. Kuchunga pia forests, hii forests Mr. Chairman maoni yangu sikupeana kwa central government, ni kutoa kupeana kwa wananchi ili watu wa Kerio wanajua forest yao ni hii, wanachunga kwa maslahi yao. Kwa ajiri yao wanajua na central government kazi yake ni ile technical provision, ile ya kusema tupande miti namna hii namna hii lakini utunzaji hata ukisema nataka kukata sehemu fulani iwe kwa shule, iwe na mahitaji ya wananchi, wawe wanachunga, wawe na county council, wawe na uwezo, wachunge forest yao, maana hii forest ilikuwako tangu zamani. Miti wazee wanajua ni miti gani inachunga nchi na nini. Na hiyo utawala nikienda juu tena Bwana Mwenyekiti, constituency iwe na mjumbe ambaye anachaguliwa na watu.

Kuchaguliwa iwe uhuru na huyo mjumbe aende kwa miaka tano hiyo – kutoka huko tuwe na President ambaye tunachagua sisi kwote pamoja. President awe kwa miaka tano ili ya kusema after two terms ya President Bwana Chairman, mimi napinga hii kwa sababu uongozi, huwezi kutoa watu kama hivi hivi, huna store ya kuweka viongozi kusema mi nawakili wakitoka 5 years, two terms naenda kutoa huyu. Kama President Moi tungewacha bado ya term mbili, hii Kenya haingekuwa vile iko. Sisi wengine tulisomea wakati wake, tumefanya kazi wakati yake, mpaka sasa tumeenda retire wakati yake. Tunataka watoto wetu pia wafanye kazi peaceful environment na grand children pia. Kwa hivyo mimi napendelea, kulingana na uwezo ya mtu, na awe achaguliwe kulingana na uwezo wake, akionekana hawezi, basi wananchi wana-vote yeye out, hiyo inatosha. Na hii system ya wakati huu iongezwe, iwe na Prime Minister, President awe na Vice wake, ambaye anatoka kila mkoa. Kila mkoa uwe na vice president, ili kutawala iwe kamili, balanced. Na prime minister awe na executive powers ili nchi ipate kuongozwa.

Na nikirudi tena kwa hali ya culture, nikisema ili nimalize, culture values ndio imechungu sisi mpaka wakati huu. Wakati huu tunaona imeanza kupotea kwa sababu watu wameanza kusema sisi tukae vile tunapenda. Apana, culture iwe culture, rika iwe na heshima ya rika ingine, tuko na rika, tukifika mahali fulani, watoto hutahiriwa, vijana apana wasichana. Wasichana wanakumbaliana na mtido wa sasa ya kwamba wasichana wa kae. Wavulana watahiriwa lakini si kila mtu atahirishe mtoto wake kwa jikoni na kuweka jikoni. Inatakiwa ile rika ya sub location, wawe wakiangalia, na tosha, angalia nyota ile ya nchi, kuna dariri fulani fulani. Kuna wakati mwingine huwa ni mbaya, apana tahirisha watoto kama hewa ni mbaya, tahirisha hawa wakati hewa ni mzuri na hio inatokana na nyota; unaangalia nyota ya nchi, unaangalia nchi kama iko chakula, kama iko nini, na watahirishwe kulingana na ratiba hiyo – group, na heshima iwekwe. Kijana akishatahiliwa ajue ametahiriwa, amekuwa mtu mzima, achunge heshima. Na hali ya wasichana wakae, hali ya wasichana kupeanwa, kuolewa ni kawaida. Lakini si kawaida ya kwamba watakuwa wakiolewa kila wakati. Kwa hivyo kulingana na mimi kama mzazi, ningependa watoto wangu ni watoto wangu. Kama moja ana kwama, apana olewa, shamba mi nakata kidogo napatia yeye. Hiyo ni shamba yangu, na hao ni watoto wangu, apana tupa watoto. Na wale wataolewa ni sawasawa lakini kupea hiyo shamba iko right ya wazee kuchunga, hakuna mtu kwisha kama huyu msichana yangu analeta mtu, basi hiyo shamba iko under the name ya family. Pana iko name ya huyu foreigner ambaye anakuja kuishi na yeye. Huyu mtu analetwa, lazima akae kulingana na desturi yetu. Akifanywa mambo baya baya, awe divorced kulingana na sheria. Msichana asiwe divorced kila wakati peke yake, hata mwanaume awe divorced.

Yule mwanaume ameenda, sio mwanaume ambaye amekaa kwa _____ kama mimi, mimi niko nyumbani, nakuwa divorced niende wapi? Lakini yule mtu ambaye amekuja kuishi _____ kwa sababu ya msichana yangu na kuchukua shamba yangu atakuwa divorced akicheza. Kwa hivyo hiyo kulingana na ile desturi yetu, culture iwe maintained. Oa kutoka familia hii, apana oa kutoka hii, hiyo ni kawaida, apana enda kuoa ovyo ovyo, hawezi enda kuoa msichana ya mhindi ama ya mzungu, _____ hiyo nikusema unakuja kuanza, naye wazee watafanya kitu kidogo kidogo watasema may be kumaanisha ya kwamba pengine awe posted halafu pengine miaka ingine tutafuata hiyo, I mean tunaenda kwa hiyo kuleta, wazungu tukileta hapana mbaya lakini oa kulingana na ujarii ile wazee wanasema. Hapana oa kwa hii, hapana oa kwa hii, si vizuri kuoa sisters, si vizuri kuoa kutoka uncles, nini, hiyo ni kawaida maana watu wanaweza kuharibika kwa kila hali yao ya tabia.

Basi hali ya dini bwana chairman, wawe wawe na freedom ya dini, mtu akae kulingana na vile anapenda, ukiwa Mkristo, kanisa gani anafuata, aende hiyo na akibaki kama ya nyumbani wazee nafikiri yao wako na tabia yao ya kusema sisi tunakaa tunachunga, heshima ya Mungu ni mingi, wanaogopa Mungu. Hiyo wakubaliwe.

Hii freedom ya express, its wrong, iwe limited, freedom ya express, ya mtu kuandika maneno chafu kwa mtu, unakuta mtu anaandika hata anasema fulani kama mimi nikiongea lugha ya kikalejin kwa hapa, mtu mkalejin anaweza kutafusiri kwa mtu mwingine anaenda anamwambia Komen alisema hii. Hiyo ni uongo.

Com. P. M. Wambua: Bwana Komen malizia malizia, tayari tuko na watu wengi.

Komen: Basi wacha nimalize bwana mwenyekiti, hiyo freedom of expression iwe limited. Also democracy iwe limited, isiwe kila mtu aseme vile anapenda. Apana, iwe respected to an extent, democracy ya kila watu.

Com. P. M. Wambua: Kama hujenda Bwana Komen kuna kidogo maswali ningelipenda wewe ufafanue maneno fulani. Kwanza ulisema ungelipendelea chiefs waendeleo kufanya kazi na subchiefs_____wawe nazo, lakini sana sana kunatokea wakati ambao hawa machiefs wana-abuse office ama wanatumia madaraka yao vibaya. Ungependekeza nini ndio tuhakikishe ya kwamba wakipewa hizo nguvu hawatatumia vibaya?

Ya pili, ulizungumzia sana mambo ya county council na sikusikia pahali unataja municipal council, ungelipendelea municipal councils na town councils ziwako ama nini? Kuwe na county council peke yake?

La mwisho ni question ya Terms of the President, ulisema, President kusikuwe na limit ya terms, aendeleo tu. Lakini kitu kimoja tulikuwa tunataka kusikia juu yake ni kama kutakuweko na retirement age ya President. Ni kweli ninaweza kusema terms, ihesabiwe, lakini kuna age fulani atafika iwe sasa sheria inasema utasimamia hapo, ama iwe open, hata akifikisha miaka mia moja anaendelea tu?

Komen: Asante sana, naweza kubuko hayo Bwana chairman asante. Ile kwanza ya chiefs, wakiabuse office kuna elders ambao watareport yeye kwa Provincial Administration. Wenyewe waseme huyu chief amekuwa ineffective na awe reported, aambiwe, halafu wenyewe wata-sort out how to discipline that chief ama wachague mwingine.

County councils isiweko na municipal councils pia na city councils kulingana na ratifa hiyo.

Ya President: President kulingana na afya yake, kulingana na bado yuko normal, bado yuko na uwezo, unajua mpaka miaka karibu themanine na tano hivi, mtu ambaye ata katika kikwetu hapa, unaweza kupata wazee wa miaka themanine na tano na bado akili iko timamu. Asionekane bado mpaka hiyo miaka ya themanine na tano bado yuko na akili timamu anaendelea vizuri effectively ifike hapo na mtu alitire kwa hapo. Asante. Asante sana Bwana Mwenyekiti.

Com. P. M. Wambua: Thank you very much Bwana Komen. Peter Kiboen nilikuwa nimetaja jina lake. Taja jina yako na utupatie maoni.

Peter Kiboen: Jina ni Peter Kiboen. Maoni napeana ni opinion yangu tu.

Kwanza ni mambo ya madini. Ikipatikana katika community fulani hasa kwa hapa Baringo kwa sababu hii nchi yetu, kubwa ni _____, mawe, sasa tukipata ni madini, mimi naonelea hiyo industry, It takes a lot of interest on the local people and this should be changed in the law. That employment kwa wale watu wanatoka hapo lazima wapatiwe priority ili mambo ya general

development- infrastructure, kama ni barabara, maji, electricity, telephone, na mashule na hospitals hawa watu wasaidiwe. Na ya mwisho hapo, ikiwezekana local people should be compensated. Wapatiwe mahali pengine pa kuishi mahali pengine, kama itakuwa madini ya kuchukua land kubwa.

Ya pili ni inheritance, na ni mtu tu amesema hivyo. Kwa sisi ni watu wa Baringo, mali inapeanwa kwa vijana na wasichana wanaolewa lakini pengine msichana mwingine amezaa nyumbani bila kuolewa. Kwa hivyo mimi naonelea hii iwekwe kwa sheria, sisemi hivi, huyu msichana amembaki, apatiwe mali kama hawa vijana wako nyumbani, na kulingana na desturi yetu, hataishi katika hiyo land ya familia. Ata anaweza kununuliwa shamba pahali pengine kwa sababu hawa watoto sio wa hiyo familia ya msichana.

Kuhusu land also, taking over of a community land na serikali, I will state, I'm proposing that if it is important that the government has to take that piece of land, and then it has got to come also into terms with the elders and the local leaders, they must talk and understand each other and see the importance of that land being taken so that there will not be some kind of _____. _____ na mambo kama ya tourism, _____ and so forth. So mimi ningetaka watu wawe satisfied as per law and they are good according to the executive where possible.

Kuhusu land also, mimi ningenelea wale wamepata land kubwa katika nchi hii, and its very potential, in production, should be made to utilize that land and cause proper production all over the land. Failure to do that one I see no reason why that land should not be taken by the state and given to other people even if it is on your ownership. There must be some kind of insecurity in the law to do that.

Now I'm coming into the high ranking of the provincial administration right up to the head of state and I will start by saying: maoni yangu ni haya, mimi ningetaka wale wako kwa hiyo offices, kutoka chief, mpaka provincial headquarters, wawe watu elected. Nasema hivi kwa sababu katika hii stage yetu tumekuwa na corruption kubwa sana ambayo tunajua, inajulikana, kwa dunia yote. Ata saa ingine we are being lugged somewhere among the top, na mimi nafikiri watu wakielektiwa _____ kwa muda fulani kama miaka tano, then wale wanafanya kazi ya muhimu watajulikana wakati watarepeat tena election. So this is why I'm saying, we need to have governance, a provincial level and this governance should be electable every five years. Say

the man who is leading the district – I could have said that admiring that the DC should be elected, those with _____ or something like that and all the personnel that are within the district will not need the security have got to revert and _____, judiciary, security, and all departments for that five years. I believe this because I tend to think that this elected person atakuwa akichunga hiyo miaka yake tano, afanye kazi clean, halafu sasa wale watu watakuwa wakifanya corruption kama vile tunaonanga tukiingia kwa matatus. Hatakuwa na

Interjection

Com. P. M. Wambua: Na Kiboren fupisha maneno maanake tupeane nafasi.

Kiboren: Okay, I think I will will be very quick So that is what I'm recommending. As for the Head of state, I also believe that they have to be elected for the five years period and at the same time we have to have a limit for the head of state because anything has to have a limit. So whatever limit have to be reached at, it should be a limit that will be convenient for him to rule and then you will have to hand over to other people.

As for any mistakes in the country right now we see that the Head of state is above the law, I believe the law should be made in such a manner that possibly if somebody is in that office, and then he has a lot of excesses (kufanya makosa mingi) and then he has to be impeached and taken to the court of law for punishment. So whoever takes the ushukani kama Head of State will always be morally upright and physically upright.

And for the election of the councillors, I maintain that the people to be elected should be above form 4. Same applies to the Parliamentarians. There shouldn't be any, so that we now operate kwa level ambayo watu watakuwa wakielewa ni vitu gani inaendelea katika hiyo constituency. Mayors na chairmen wa councils should also be elected by the whole district nd the township so that he becomes a mayor for all the people. Chairmen for the council for the whole district

Interjection:

Com. P. M. Wambua: Apana, time imeisha, vile utafanya juu naona uko na memorandum hapa, utatupatia na hiyo memorandum tutaesoma. Nafikiria yale ya muhimu yote umeyataja, kwa hivyo utupatie memorandum halafu tutaenda kuisoma.

Kiboen: I will do that because I have already written I will give you this.

Com. P. M. Wambua: Asante sana. James Kiprop, yuko? Councillor Isaac Chemobo or Jemobo. Taja jina vizuri halafu utupatie maoni.

Councillor Isaac Chemobo: Mimi ni councillor Isaac Chemobo kutoka Oseo location.

Interjection

Com. P. M. Wambua: Tafadhali fupisha maneno naona umembeba memorandum mrefu sana. Kwa hivyo tafadhali adika yale ya mhimu dakika ni tano tu.

Councillor Chemobo: Asante bwana commissioner. Ya kwanza, Katiba hii tumepokea na tunasema asante ili tutoe mapendekezo yetu. Tunapendekeza ya kwamba bunge ikikutana kwa uwaja fulani, ili ipitiswe, ile 65% iongezwe kuwa 69% .

Uraia: Tunaomba Katiba iwekwe ili mwanamke yeyote ambaye ataolewa na mtu wa Kenya, awe raia automatically.

Usalama ya nchi ipewe Rais kama kawaida.

Vyama vya siasa ifupishwe kutoka ya wakati huu 43 au 47 mpaka 3 kwa sababu vyama zikikuwa mingi, itagawanya wananchi wa Kenya.

Miundo ya aina ya serikali: Wakati huu tungependekeza miundo ya serikali tuwe na Rais kufika head tuwe, na waziri mkuu na tuwe na serikali ya majimbo.

Mahakama: Tungependekeza Katiba iundwe kwa upande ya mahakama, korti isisikize kesi ya mashamba kwa sababu kule kortini, hawajui mipaka yetu, irudishwe kwa wazee wa mitaa, assistant chief, na chief na DO ili watu wale hawajiwezi, hawawezi kufika Nairobi.

Serikali ya mitaa: County council au mtu akiwa councillor mpaka awe na masomo ya darasa la nane mpaka University. Wale wanahitaji kuwa mayor na vitu vya county council, lazima wawe na form 4 na kwelekea juu.

Haki ya kimzingi: Elimu – tunataka Katiba iwekwe ili masomo iwe free kutoka nursery mpaka kidato cha nne. Na serikali igalamie school equipment kama zamani.

Haki ya Ardhi na mali: Tunaomba Katiba iundwe ili serikali lazima ilipe compensation kwa wale ambao shamba zao zitachukuliwa na serikali. Wanaume na wanawake wawe na uwezo wa kumiliki ardhi. Katika sheria zetu za Tugen au mila zetu, msichana hawezi kupewa shamba na tungependekeza iseme hivi, ile familia ambayo haikujaliwa kupata kijana, aruhusu msichana aamiriki shamba. Mtu yeyote ambaye anaye shamba hatumii kikamilivu tunaomba Katiba iwekwe ili hiyo shamba ipate kuteuliwa na serikali na kugawanywa wale ambao hawana.

Pade ya ardhi kwa ukulima: Katiba iundwe ili price control iletwe, mfano, price ya mahidi mbegu, mbegu ni bei kali kuliko ya kukula. Kilo kumi begu ni shiringi elfu moja mia tatu ishirini na ile ngunia moja ya 90 kilo ni shilingi mia tatu mpaka mia nne. Katiba iangalie hiyo mambo.

Haki za wana jamii: Kutahirisha wasichana ipigwe marufuku lakini vijana iendelee vile ilikuwa. Katika sheria zetu za Tugeni, kijana mkubwa ndiye atakayemshika baba wakati atafaliki na yule kijana mdogo amshike mama. Tungependa Katiba imruhusu jamii yake imushike au ifanye mashizi kwa watu wao, sio kwa binti yule analetwa kutoka nyumba ingine. Tena tungependa sheria ya kuweka mtoto kiboko irudishwe kwa shule watoto wawekwe kiboko. Hata kwa bibilia kwa kitabu cha Methali 22:15 inatwambia kwamba lazima mtoto aoje kiboko akikosa.

Com. P. M. Wambua: Councillor tafadhali fupisha maneno maanake hiyo memerandum tutaisoma.

Councillor Chemobo: Ninaenda kumaliza, kwa desturi yetu tena ya tugeni, hatuna divorce. Tunaye separation, yaani mtu akioa bibi yake, wakati wanakosana hakuna kufukuza yeye aende kwao. Anajengewa nyumba kule na anakaa kama bibi yako

lakini mzungu alipokuja akasema wacha hiyo bibi arudi kwao. Kwa hivyo tunataka hiyo iwe sheria ya kwamba kama umeshaoa, umeshaoa weka yeye kando kule aendelee awe bibi yako hata kama utakosa kwenda kule.

Ya mwisho: masirahi ya walemavu iangaliwe. Watoto wao wapate kutunzwa na serikali kuanzia primary mpaka university.

Urithi Upokesanaji wa uwezo; Rais yeyote amestaff apewe ulinzi, mshahara na asishitakiwe katika mahakama yeyote akiacha kazi. Asante bwana commissioner.

Com. P. M. Wambua: Thank you very much councillor. Please register your memorandum there. Your views are very good, we will take them into the account. Tunamuita Jacob Chetalang. Hayuko? Charles Chepchien, He is not there? Tutamuita Bin Sein Kirop. Hayuko? Joseph Cherop, Joseph Cherop, yuko? Joseph Cherop, ameenda? Samuel K. Kale.

Samuel Kiptui Kale: Asante sana commissioners kwa kupata nafasi hii. Yangu neno la kwanza ni juu ya elected leaders. Jina ni Samuel Kiptui Kale. Ningependa kuongea juu ya elected leaders ambao wanatoroka watu wao baada ya kuchaguliwa. Hawa watu kuwe na sheri ambayo wakipotea kwa muda fulani waondolewe kwa uongozi kama vile nasikia hata bunge akikosa siku nane anaondolewa. Kuwe na sheria ambayo itasaidia kuondoa watu kama hao. Wasiwe wakikula pesa na huku hawasaidii watu.

Neno ingine ni juu ya minerals ambayo inapatikana kwa nchi. Tunasikia sheria ilioko sasa ni kwamba chochote itakapopatikana chini ya ardhi inch sita si mali yako ni ya serikali. Na wale wakaaji wa sehemu hiyo, watakuwa wakiona mali ikienda na hawapati chochote. Ningependa kuwe na sheria ambayo wale watakuwa wakifikiriwa watapewa nini au kuwe na society fulani ambayo itasaidia hawa wapate mali hiyo.

Ingingine ni mambo ya communication: Katika Katiba iliyoko sasa, tunaona sehemu zingine hakuna barabara, hakuna simu, na hali wakati wa Hata mali kugawanywa mali kwa serikali kufanyia maendeleo, sehemu kama hizo zimesahauliwa. Kwa hivyo kama Katiba itakuweco itasema sehemu kama hizo isaidiwe ama mali ambayo ni ya nchi iwe ikifikia sehemu kama hizo kwa kutengenezewa barabara na hali ya simu. Communication kwa jumla.

Mambo ya free education: Kuna sehemu nchi kavi ambayo watu hawana mali na wangehitaji watoto wao wasome, tungeomba Katiba ya Kenya iseme ya kwamba, watu kama hawa wawe wakipewa free education mpaka darasa la nne ili kila mtu awe na elimu sawa katika nchi.

Nyingine ni juu ya afya: mfano juzi kulikuwako na immunization ambaye ni ya misciles, pengine kuna sehemu ingine haikufikiwa kwa sababu imekuwa bali hakuna barabara hakuna hata hospitali. Sehemu kama hizo ziwe zikifikiliwa katika Katiba hii mpya ya kwamba ifikiwe sehemu zote katika mambo ya afya kama vile Katiba ya mbele inasema tulitaka kuondoa ujinga, ugojwa na umasikini. Na wanakuaga pengine hiyo Katiba haikutimiza *End of side A tape 3*

Councillors katika nchi ya Kenya wawe wakilipwa kama wabunge kupitia national assembly kwa sababu county council inaonekana mara kwa mara tunasikia councillors wanalia hawana pesa kwa sababu council yao hakuna pesa. Iwe kwa sababu ni viongozi wanachaguliwa na wako na wananchi zaidi kuliko hata mbunge, pesa yao itoke kwa national assembly kama vile wabunge wanavyofanyiwa.

Mambo ingine ni koti: Local authority wana charge koti pengine mimi nikiwa mfugaji, ninafuga ng'ombe yangu kwa shinda mingi lakini wakati napeleka auction nakuta mtu hapo anataka koti na ikiwa n hivyo, local authorities wawe wakisaidia kama ni wafuganji, wasaidiwe kwa njia zingine kama madawa ya kutibu ng'ombe zao na wawe na madaktari ambao watakuwa wakiangalia masirahi ya hizo mali ili kesho tukilipa koti tunajua tunasaidiana na hawa. Kwa mfano, kama wakulima wa mashamba, mtu anafuna mahidi yake anaweka store anakula sawa sawa, hakuna kodi analipishwa. Hawa wakipeleka soko kama hapa pengine hakuna kodi analipishwa lakini mimi nikileta ng'ombe yangu kwa sokoni nadaiwa, inakuwa black _____ kama nitauza elfu mbili ni _____ na yule ameuzia elfu ishirini. Hata hapo hakuna usawa. Kodi pia kwa biashara hizi dogo dogo kama viosk, maduka, unakuta pengine, katika Katiba, haitabui ya kwamba yule ana ifaa katika duka lake ya shiringi elfu ishirini, na yule anaprefer ambaye ni elfu mia moja. Pengine nadaiwa kodi inakuwa sawa. Tuwe na tofauti hapo ambaye ni kama vile hii mambo ya Value Added Tax. Mali ya mtu iwe valued ndio indaiwe kodi.

Ya mwisho ni mambo ya kazi. Kwa wakati huu tunaona watoto wamemaliza mashule, wengi wao wako barabarani wakitafula kazi. Katika Katiba, iwe kuna njia ambayo kwa mfano kama National Youth Service, iwe ni compulsory ambaye watoto watakuwa wakipitia huko wakimaliza secondary education wale hawakuweza kwenda university. Wapitie mahali fulani ambao watakuwa wakipata mafunzo – courses bali bali halafu kuwe na record ambayo kuajiriwa nafasi za kazi hizo zikipatikana wanajulikana wako. Nafikiri hayo ndio ni nayo. Asante sana.

Com. P. M. Wambua: Asante sana. Tafadhali jiadikishe hapo. Tunamuita Mama Damaris Chereko. Ako wapi Damaris? Damaris Chereko – Kenya Women Political locals, Johana Kibet, Johana Kibet .

Johana Kibet: First of all my name is Johana Kibet. Mr. Commissioner, the first point is the council of elders who deal with issues in our communities or sublocation should be recognized by the government and be paid. Everybody in Kenya regardless of position and authority should be charged equally. The powers of the President should be reduced and the ministers should be chosen by the cabinet.

Anti-corruption authority should be formed and should have a right to prosecute any corrupt person found receiving or giving bribes.

In terms of education, the government should prioritize the needy children who come from poor backgrounds for burseries and should be clear from the routes. The parliament should not be extended since the law states clearly that a term that is 5 years there should be an election which should be done to elect new leaders unless there is crisis like war. That is when the life of the parliament will be extended but in Kenya there is no crisis. Those are the only ones.

Com. P. M. Wambua: Asante sana, thank you very much. Ezekiel Tuigon.

Ezekiel Tuigon: Thank you commissioners, my name is Ezekiel Taitu Tuigon. I have come here with some few points to make.

Ya kwanza ningependelea kutaja juu ya muda wa serikali. Mimi ningependelea tuwe na muda wa serikali wa federal system of government. Hii ni mana ni serikali ile ya majimbo ambapo itahakikisha ya kwamba rasilimali zote za nje zinagaiwa sawa kwa

Charles Toroitich: I'm sorry please, minimum ni 5 acres. Maximum can be as much as you can utilize. Unaweza kuwa na shamba, unapanda vitu kama kahawa ukiwa Nyeri ama Kiambu. Large scale farm.

Com. P. M. Wambua: Okay tumeelewa sana hapo bwana Toroitich. Asante sana, thank you very much kwa yako ambao mazuri kabisa. Sasa tumepata mwingine tulikuwa huyo ndiye wa mwisho lakini tumepata mwingine Wesley Cherop. Ako wapi? Alikuwa amechelewa kidogo lakini tutampa nafasi. Cherop taja jina hapo na utupatie maoni kwa kifupi. Sasa kabla hatujaanza na Cherop, kuna mtu hapa ambaye alijiaandiksha na hajaitwa kutoa maoni? Wako wapi? Waje hapa mbele. Wapatie nafasi hapo. Wapatieni nafasi hapa tumalize na hawa ndio... hapo hapo hapo ndio niwambie vile tutafanya tafadhalini. Hata mama? Mama ndiye utanza. Mama wewe ndiye utanza kama unataka kutoa maoni. Kwa hivyo Basi hawa sasa ndio tutamalizia na wao. Wa mwisho ambaye alikuwa amejiandikisha hapa ni Bwana Cherop. Kwa hivyo tutaanza na Bwana Cherop halafu ndio sasa tutaanza na mama pande ile, halafu tuje namna hii tuishie hapa. Na mkija hapa tafadhalini msembe yale ambayo ya kusemwa. Kama jambo limezungumzia na limetajwa na likaingia kwa machine na tumeandika, usirudie. Lakini kama

ni kuja tu kusema hiyo jambo ni moto moja lazima tulitaje, taja tu kwa nusu dakika halafu tumalize. Kwa hivyo Cherop endelea hapo halafu tumuite mama.

Wesley Cherop: Asante sana mimi ni Wesley Cherop. Bwana commissioner kile itu mimi ninasema, asante kwa kukuja tarafa ya Kabartonjo kusikia maoni ya wanachi. Sisi ni watu young bus tunangojea vile nyinyi uamuzi yenu inaenda. Basi maoni ile kitu mimi nataka kusema, ni maneno ya kazi watu wakimaliza shule, wako nyumbani, wameingia kwa maneno ya busaa, pombe, nimi, na

Interjection:

Com. P. M. Wambua: Unataka je?

Wesley Cherop: Kitu ile mimi nataka ni kama iko vacancy ama kazi yeyote ile wanaweza pata, waandikwe.

Maanake Katiba ya sasa, mimi nasikia _____ aseme namna gani, lakini mimi naona sisis tumekuwa tukijali nini, nini, kwa sababu uchumi umeenda chini saa ingine.

Com. P. M. Wambua: (inaudible)

Wesley Cherop: Ya pili kitu ile mimi ninasema, kuna watu wameandikwa Kenya. Wako sasa wanafanya kazi wako over age almost 60 years, 65 years, 55 years, na siku ingine wako nyumbani. Wawe waende retire wahesabiwe pesa yao waende nyumbani na wengine waandikwe.

Com. P. M. Wambua: hawa ni old turks?

Wesley Cherop: Ee old turks.

Com. P. M. Wambua: Unataka waondoke au anmna gani?

Wesley Cherop: Waondoke ndio young turks waigie.

Com. P. M. Wambua: Okay, jambo la tatu Bwana Cherop.

Wesley Cherop: Jambo la tatu tunataka maneno ya shamba: Kuna mtu amesema maneno ya shamba lakini mimi sioni kama hiyo shamba iko kwa sababu wakubwa wakubwa wamechukuwa hiyo mashamba – almost one thousand acres, two million acres lakini mtu anachukua hiyo?

Com. P. M. Wambua: Ungelipenda tufanye nini?

Wesley Cherop: Hiyo, proposal yangu sasa ni hiyo maneno ya shamba hiyo, kama hii Katiba inasema ikiwa mtu hasemi nini, yangu mimi binafsi, mimi ni mtu wa Kenya na nimezaliwa Kenya. Hatutaki maneno ya kula watu wanakula mbele halafu mabaki inaingia hapa.

Com. P. M. Wambua: Cherop tupatie proposal. Ungelipenda tufanye nini?

Cherop: Tubadirishe vitu ziwe new. Kama unakuwa

Interjection

Com. P. M. Wambua: Nataka kufuatilia jambo hii la shamba, ulisema haiwezekani maanake wakubwa wako na wamechukua na hakuna. Ungelipenda tufanye nini kwa hiyo jambo? Tuambie.

Cherop: Hiyo proposal ni kama imepangwa, kama ni Baringo, apate kama acre tuseme elfu hamsini, aende kwa wenye hawajiwezi. Kama ni mtu hajiwezi hana shamba, apewe hata two and half acres, five acres, hiyo ndio itasaidia hawa.

Com. P. M. Wambua: Cherop, wewe unapendekeza ikiwa kuna ardhi inatolewa wasipewe matajiri, wapewe watu wanaositahili kupewa kwa sababu hawana ardhi.

Cherop: Ya.

Com. P. M. Wambua: Basi

Cherop: Ipewe wenye hawajiwezi, halafu hao maofficers wanatumia pesa, watumie pesa, kama ni shamba, alete shamba pande hii.

Com. P. M. Wambua: Jambo la nne.

Cherop: Ya nne ni maneno ya ufisadi (corruption)

Com. P. M. Wambua: Endelea.

Cherop: Mimi nilikuwa Nairobi hata mimi. Nilisikia vile watu wanaongea sio watu – tusema hawa watu wameokoka, kube hakuna wakubwa. Vile mimi nataka ni kusaidiana. Kama ni mwingine ako na cheo fulani fulani mahali fulani wasaidie wengine.

Com. P. M. Wambua: Proposal ni nini hapo?

Cherop: Ya hapo ni kusema hii mabadiriko ya Eh eh

Interjection

Com. P. M. Wambua: Ujue inarecordiwa tu. Tupatie proposal.

Cherop: Sasa, kitu iko kwa upande wa kwetu hapa tuko nyuma sana. Hiyo mashamba serikali imetusongesha mpaka imemaliza shamba kabisa. Hakuna shamba. Hata nikikupeleka saa hii Bwana commissioner huko nyumbani kwangu mimi napanda wimbi na sijui kama nitaweza kula mwaka huu kwa sababu hakuna _____.

Com. P. M. Wambua: Ulimaliza mambo ya land ukasema serikali ihakikishe kwamba wale ambao hawana mashamba

wamepewa, halafu kutoka kwa shamba, ukaingia kwa corruption, ukasema ufiada, sasa ukataja ufiada na ukarudi kwa mashamba, ufiada unasema tufanye nini? Corruption?

Com. Abubakar Zein: tena ukasema ulienda Nairobi ukakuta watu wengine wanasema wameokoka lakini hakuna wokofu?

Cherop: Yee, hakuna wokofu, kwa sababu *end of tape 4 side A*

Ufiada haiko ndio tupate hata kazi.

Com. P. M. Wambua: Haya, ya tano bwana. Kuna lingine lolote umebakisha?

Cherop: Ya mwisho ni maneno ya general election. Iisemekana ati inafanyiwa mwisho ya mwaka huu na tumesikia inafanywa.

Kitu ile mimi nataka ni ifanywe the end of this year kwa sababu itaenda mpaka mwisho wa mwezi wa tatu kwa nini?

Com. P. M. Wambua: Kwa hivyo election ifanywe mwaka huu?

Cherop: Mwaka huu.

Com. P. M. Wambua: December?

Cherop: Yes, ifanywe.

Com. P. M. Wambua: Basi, ya sita bwana.

Com. Abubakar Zein: Alisema ni la mwisho.

Com. P. M. Wambua: Lile lilikuwa la mwisho?

Cherop: Eee.

Com. P. M. Wambua: Haya basi tumeandika hiyo election on time December.

Cherop: Isiende mbele.

Com. P. M. Wambua: Haya. Asante sana bwana Cherop. Mama tafadhali kuja hapa. Taja jina na utwambie yale ambao hayakusemwa. Kama yanalingana na akina mama tutajie tafadhali.

Priscah Chepsengei: Kwa majina mimi ni mama Prisca Chepsenge. Bwana commissioner sir nitazungumza kwa kilugha.

Priscah Chepsengei: *Amwae commissioner alenchini ne amache kinde Katiba ko en achek Tugen, desturi yetu nebo Tugen ko wakati msichana, wakati tunaenda kupoza msichana, ko Commissioner ko kimoche kende Katiba kele sait ne kakibe kebe koito, ko ye kakebe koito ko kimoche kende Katiba amun ye kibe koito ko moginoe kele tos wo kotun weri chebi anan ko mayachin harusi ko kimache kele sait nebo koito kinde Katiba kele nyoru certificate kony'eten sait no bo koito.*

Translator: Tungetaka kwa mila yetu wakati tunapo-oa kama vijana, wazee wanaenda kwa pale msichana yuko na wanaongea na wanaelewana. Na tunapenda Katiba ieleze kwamba siku hiyo wakati hiyo agreement inafanywa hata certificate ifanywe kwa sababu ni masikizano ya kamili.

Priscah Chepsengei: *Amun ki kere kele saisiek alak kimoche kende Katiba ku non amun sait age ngwo lakwet komuche agot ye kakeba ng'alekab divorce kemuche ke-divorcen ak kowo buch ama kinae kele tos betut ne kikibendi koito ko kikisir nee, so kimoche kinde Katiba kou non.*

Translator: Nasema hivyo kwa sababu, mara baada ya muda huyu mume anataka kufanya divorce lakini wakitaka kujua wakati ule walifanya kuposa mtoto, agreement ilifanywa namna gani, haielezwi, kwa hivyo inaleta tatizo.

Priscah Chepsengei: *Ya pili amache amwa agobo kinde Katiba ng'alekab wazee anan boisiet. Betusiechu kekere kele king'et muren ko bisto responsibilities chekwache cheyoe en gaa, kobibisiyi kityo wamama. Ingen kole mi lagok, kiyagik, mi tugul tugul che katoyoei, mi agot karwa ne katokerei, mi kasisiek tugul chebo muren ko lakini mi tuguk che mayaei mama, che mamagat en sheria chechok chebo Tugen lakini kikere saisiek alak motun agot isoru chepyoso ile*

kilany kosyep kot ago kilen keshep kot ko ma sheria chechok cho.

So kimoche kende Katiba kele muren age tugul ne ingen kole a chi muren ne murenot koyai kasinyin komamge ak murenotenyin.

Translator: Kulingana na mila yetu kuna mambo ambayo kazi ambazo mume hufanya kwa nyumba kama kuzeeka nyumba kupanda juu na mama _____ lakini kwa wakati huyu wazee wamewacha kazi zao – hizi responsibilities zao. Tungetaka Katiba ieleze kinaganaga vile wazee lazima wafanye halafu akina mama wasiende kufanya ile kazi halafu mila isiwaruhusu.

Priscah Chepsengei: *Nebo somok ko amache amwa upande wa wamama amache amwa ale wakati ne mi uchaguzi nebo wamama, amache amwachi wama alenji wakati huo kemoche keroo mama ne kichakwani ko mama ne tinye mfano mzuri kong'eten gaa agoi ne ribe lagokyik, korib boisionikyik en gaa, kemuche huyu mama kemuche koek kiongozi ne kararan amu iborto mfano ne kararan. Si makibe ngemi katikati olon ye kiro ne kilachge, keo netinye rabia, kekwai anan keroo ne tinye kaitanywan kook, kekwai kou kaitanywan. Kimoche kekwai mama ne tinye mfano kong'eten gaa ako family che chiche komi gaa tugul.*

Translator: Tungetaka Katiba ieleze vizuri uchaguzi wa uongozi ya akina mama. Kwamba mama ambaye atachaguliwa kuwa kiongozi ni mama mwenye heshima, mwenye nadhili nzuri ambaye anahesimiwa nyumbani ambaye akitegeleza wajibo anategeneza ile inapendwa. Si kwamba waone wale ambao wamejifaa vizuri wale wana watu wao, labda na wanatoka kwa ukubwa, hao wanatoka mahali wamesoma, Ee, apana, lakini ni mama yule ambaye ana hekina anastahili kuongoza.

Priscah Chepsengei: Thank you very much sir.

Com. P. M. Wambua: Nilikuwa naambiwa ianze kule inaishia hapa, sasa wewe unaanza huku . Mzee utaje jina, halafu utuambie maneno yale ambayo hakusemwa hapa, yale mapya.

Jacob Cheptaalam: Mimi ninaitwa Jacob Cheptalam. *Mwachi anyun kole ko en ng'akekab katiba ko kikimi achek koroni komite bik alak che kilelach. Kou ye kokwan commissioners, kimi bik alak che lelach koroni.*

Translator: Kama vile nyinyi wanacommissioner mumefika hapa leo, mimi nilipokuwa mdogo niliona wale walikuwa wazungu, watu weupe walikuwa upande huu.

Jacob Cheptaalam: *Ko en yoton ko kikiyochin achek kasit.*

Translator: Tulikuwa tukiwafanyia kazi.

Com. P. M. Wambua: Fanya hivi mzee, hata wewe, just get the idea which he want to communicate to us, translate and tell him what we want is proposals. Atupatie proposals in respect of issues which have not been stated here. Ako na dakika mbili na moja imeenda.

Jacob Cheptaalam: *Ilenchin ng'olyondet ne amache, ne kaker ko ng'alekab fees.*

Translator: Jambo ambalo ninatka nilitaje ni juu ya fees – karo za shule

Jacob Cheptaalam: *Ilenchin kelipan fees raini ko kito ne korom.*

Translator: UlipANJI wa karo ya shule imekuwa jambo ngumu sana upande huu.

Com. P. M. Wambua: Mwambie mzee kuna watu wamekuja hapa wakapendekeza kwamba elimu iwe ya bure. Yeye anataka nini? Ungependa iwe ya bure?

Jacob Cheptaalam: *Kakomwa bik alak*

Translator: Ndio.

Com. P. M. Wambua: Basi hiyo imeingia. Mpaka darasa gani? Au mpaka university?

Jacob Cheptaalam: *ikiwezekana iwe mpaka university.*

Translator:

Com. P. M. Wambua: Na ya pili?

Jacob Cheptaalam: *Ya pili ko boisiokyok, chemi kazi asikobwa gaa...*

Translator: Jambo la pili ni wazee watendaji kazi lakini wameenda retire huko nyumbani.

Com. P. M. Wambua: Hiyo sasa tuliisikia tukaambiwa kwamba retirees wale ambao wametoka kazini na wamefanya retire wachungwe, wapewe allowances mpaka wafe. Unataka kuongezea?

Jacob Cheptaalam: Ndio, mimi nataka kuongeza hapo. Saidia hawa.

Translator:

Com. P. M. Wambua: Hiyo imeingia . Ya tatu mzee.

Jacob Cheptaalam: *Ya tatu ko ng'alekab kirwokik. Kirwogik ko amune si ma konech kekwai ehek eng yu.*

Translator: Kwa nini tusipewe jukumu la kuwajiri chiefs?

Com. P. M. Wambua: Hiyo sasa nilisema, na watu wakasema hapa na tumeandika chiefs na assistant chiefs wachaguliwe na watu N kama wafanye, na tena wafanye kwa mlolongo wakionekana mchana. Unataka iingie hiyo? Kuna lingine?

Jacob Cheptaalam: Ingine Ni hayo tu

Com. P. M. Wambua: Asante sana. Jiandikishe hapa tafadhali. Sasa kijana utataja jina na utwambie yale ambayo hayakusomwa.

Fred Kibet: Kwa jina ni Fred Kibet.

Com. P. M. Wambua: Kama ni kuongezea ile tunasema kuongezea uzito, useme nimekuja kuongezea uzito na yangu ni hii, hii,

na ile basi.

Fred Kibet: Yale yamesemwa hatutaongezea uzito, nitasema tu zingine.

Com. P. M. Wambua: haya asante sana. Sema jina tafadhali kwanza.

Fred Kibet: Fred Kibet, Yangu ya kwanza mimi naonelea siku ya campaign kwa bunge ama councillors wasitumie pesa kwa sababu ni kama kupeana hongo. Mpaka unabadirisha akili ya mwenye angetaka kuchaua mtu. Na hiyo isitumiwe pesa hata kidogo

Com. P. M. Wambua: Sawa.

Fred Kibet: Ya pili, saa ile tuseme mtu amefanya makosa, officer akitumwa asike yeye asitumie nguvu. Ashike kwa heshima, kama ako na watoto wake kama wanakula, askari akuje tu pole pole, akuje aombe ruhusa amwambie iko report anatakikana afikishe huko lakini sio kushika yeye mpaka watoto washtuke wapate heart failure, amshike pole pole.

Ya tatu ni political parties. Tusione party ingine ni adui tuseme KANU kama upande mwingine hakuna (ni kama marafiki tu) tusione party ingine kama ni mbaya kuliko party ingine. Yote ni yetu kwa Kenya.

Ya nne ni elimu: unakuta mtu amepita ako na points nzuri lakini hawezi kufika university kwa sababu hana pesa Lakini unakuta akikutana na mtu mwenye ako na pesa, pengine ako na C- anaenda private university na kesho ni graduate. Sasa mimi ningenelea Wakenya tutakosa mean grade tukifanya hivyo.

Com. P. M. Wambua: Sasa unataka je?

Fred Kibet: Nataka tuseme graduate should be kama ni B ikuwe B. So long as hata kama ako na pesa ama asikuwe na pesa, asiingie university kama ako na less grade.

Inginge ya mwisho ni malipo kwa wafanyi kazi: Tuseme certificate, a certificate skill B skill iwe karibu equal kwa kila ministry hata parastatals. Sio ati mtu akiwa security anashinda mtu mwenye alienda _____ kwa ingine. Salary scale ikuwe sawa per certificate.

Com. P. M. Wambua: Kuna na jambo nataka kujua, umesema ile arrest, iwe na heshima. Kuna pahali ilitajwa ya kwamba ni mzuri kama mtu anajulikana. Ukija hapa, sasa unakaa hapa na unaishi hapa na unajulikana kama umefanya makosa, vile inatakiwa kufanyika ni chief ama yule mzee wa mtaa anaambiwa, mwambie fulani anje kwa police station. Ungependelea hivyo?

Fred Kibet: Si hivyo,

Com. P. M. Wambua: Ungependelea ashikwe tu lakini ashikwe kwa heshima.

Fred Kibet: Police akuje tu kama ako na watu sio ati ashikwe kama anakula hata kama hajamaliza kula, Sasa ni hayo tu.

Com. P. M. Wambua: Asante sana. Yako yalikuwa mageni kweli. Mzee tupatie mageni pia ambayo hatukuyasikia tangu asubuhi. Taja jina na uendeleo.

Paul Cheptoo: Kwa majina naitwa Paul Cheptoo kutoka sublocation ya Kabtele na ile kitu mimi ninasema ile haijasemwa na watu ni haya:

Kuna watu walikuwa wanaishi especially kwa dani ya forest, waliacha watu wao, na manyumba yao ilichomwa na hawana shamba mahali inging. Kwa hivyo ningomba kwa hii sheria ya constitution, watu hao warundikshwe mahali walikuwa wanaishi kwa kuchunga watu wao wale waliwachia wajukuu au mababu yao.

Com. P. M. Wambua: Warundi pahali walitoka huko kwa misitu ama wapewe pahali pengine pakuishi?

Paul Cheptoo: Warundi mahali walikuwa wana ishi maana hapa kwisha a_____ mashamba yao. Kwa sababu hata sasa wameteseka. Hawana mahali popote wanakaa, wanakaa tu kwa manyumba ya watu wengine.

Com. P. M. Wambua: Hata ikiwa ni kwa misitu warudi huko?

Paul Cheptoo: Yes, warudi mahali walikuwa wamezaliwa.

Com. Abubakar Zein: Lakini nisaidie mzee, shamba liko dani ya msitu?

Paul Cheptoo: Yes, tangu babu ya mababu.

Com. P. M. Wambua: Okay, hiyo tumesikia, jiandikishe hapa Bwana Cheptoo. Ni kama wanaongezeka, walikuwa watatu sasa ni ...

Paul Cheptoo: Kuna kitu ingine ningependekeza, sijui kama hiyo kitu imeingia vizuri, unaoma kijana anaweza kwenda kwa mzee fulani, anachukua msichana (kama vile yule mama alikuwa amesema hapa) halafu baadaye anafukuza yule msichana anarudi kwa wazazi na ako na watoto. Mtu kama huyu ningeonlea afuatwe maana anajaribu kutesa watoto.

Com. P. M. Wambua: Hayo mzee alisema lakini umeyatia moto kwa hivyo asante sana bwana Cheptoo. Anayefuata hapo. Taja jina Fred halafu utuambie mapya.

Michael Cheptumo: Kwa majina ni Michel Cheptumo, kutoka hapo Simu Location. Mimi naenda tu straight forward kwa point ile niliandika hapa. Yangu zaidi ni juu ya ugawaji wa utajiri. Natoa upande moja – kwa wafanyi biashara tu. Tuko na mhindi ambaye yuko na wholesale kubwa, amebeba kila kitu, P_____ iko huko, majani iko huko, chumvu iko huko, sukari, kila kitu, so mimi ningomba commission iwekwe kwa Katiba ya kwamba usawa ya utajiri tugawe. Mtu wa kusupply sukari awe mtu mmoja, ugawaji wa chumvu iwe mtu mmoja, ugawaji wa majani iwe kitu moja, Halafu isibebe pesa zetu kwa mtu mmoja. Ukiangalia karibu kwa wholesale zote katika tarafa yetu ya Kabartonjo, hawa hata Sheik mwenyewe, utakuta ni mtu mmoja tu anabeba kila kitu na kuna watu wengi walienda retire na wako na pesa chungu mzima wamekosa kitu ya kufanyia. Nataka kwanza hii

Com. P. M. Wambua: Hiyo tumesikia.

Michael Cheptumo: Imesemwa?

Com. P. M. Wambua: Hiyo tumeisikia na imeingia tayari.

Michael Cheptumo: Asante. Ya pili, nataka mambo ya jua kali. Nataka pesa za jua kali ile inatolewa na serikali ipelekwe moja kwa moja kwa division. Halafu wana kamati wa jua kali wa division wagawane hiyo pesa kwa ili members wa division wafaulu kwa biashara yao. Lakini kitu ingine, kuna pesa ikitolewa kutoka kwa serikali inaenda kwa mtu binafsi. Tunaambiwa ya kwamba kuna mtu anaitwa NGO anakuja kusimamia ile pesa, Sasa kusimamia hiyo pesa, unaona haina usawa, unaangalia line ingine unaangalia line ingine na kwa kila ingine, maoni yangu ni hii pesa iletwe tu moja kwa moja kwa wale registered to a division. Isimamiwe na division.

Com. Abubakar Zein: Pesa ya serikali, ngoja ngoja mzee wangu, unasema pesa ya serikali huenda kutolewa kwa serikali ikapelekewa NGO igawanyiwe watu?

Michael Cheptumo: Nasema hivi, hii pesa ikitolewa kwa serikali ipelekwe (kama hata juzi imetangazwa) pesa ile itapatiwa NGO halafu wapate kuja kusimamia,

Com. Abubakar Zein: Ndio nakuuliza mzee wangu, wewe unasema, kuna wakati pesa ya serikali inatoka kwa serikali inaenda kwa NGO

Michael Cheptumo: Ni mfano kama hii ya KMF. Ililetwa kutoka kali, Batiwa division Kabartonjo kwa jua kali.

Com. Abubakar Zein: Kenya Management Assistant Programme?

Michael Cheptumo: Yah, so sisi tunaomba serikali iwekwe katika Katiba pesa iletwe kwa division. Thank you very much.

Com. P. M. Wambua: Asante sana bwana Chetumo. Naona hapo unabeba memorandum,

James Kiprop: I will just read it briefly.

Com. P. M. Wambua: Usisome, utatwambia yale ambayo hayakusemwa tafadhali. Tutaenda kuyasoma yote yale hakuna kitu tutabakisha hapo. Yale ambayo hayakusemwa tafadhali.

James Kiprop: My names are James Kiprop. My views are as follows:

The provincial administration in Kenya should be scrapped and their powers be given to the Local Government.

The administration police post should also be scrapped and their duties be handed over the police to avoid implication of services.

Human rights commission should be formed in Kenya and be given the power to prosecute those who abuse other people's rights.

Another one, the judiciary should confide a way of protecting those poor and illiterate Kenyans in court because these people can be charged unfairly.

Councillors and mayors should be chosen directly by the people.

Com. P. M. Wambua: Hiyo ilisemwa, endelea.

James Kiprop: Death sentence should be abolished in Kenya.

Anti corruption commission should be formed in Kenya and be given the power to investigate and prosecute

If a Kenyan citizen is illegally arrested and subjected to unfair treatment in a police cell, he should be compensated.

Traditional brews should be legalized as a way of preserving our African culture and at the same time assist those Kenyans who

cannot afford to buy the commercial brews.

Com. P. M. Wambua: Endelea

James Kiprop: The last point is that the parliament as we near the general election, the parliament should not be extended because we are sure that we are going to chose leaders who will continue with the same duties like the current parliament.

Thank you and his honour.

Com. P. M. Wambua: Thank you very much Bwana Kiprop. Sasa tuko wa mwisho, Utataja jina na tafadhali huyu ndiye atakuwa wa mwisho kabisa atufungie kikao. Yale ambao hayakutajwa ndio utatuambia mzee. Maanake kama yametajwa tayari, yameingia na tumeyaandika.

Ruto Kipkemei: Mimi niliingia nyuma mimi sijui kama imetajwa kwa hivyo nitasema tu.

Com. P. M. Wambua: Nitakwambia, utasema na mi nitakueleza. Endelea.

Ruto Kipkemei: Kwa majina ni Ruto Kipkemei kutoka Barto division. Jambo la kwanza ni jambo

Ruto Kipkemei: Kwanza, *ko netai, ko mi ng'olyon ne amache amwa agobo ng'alekab imbarenik.*

Tlanslator: Jambo nataka kuliguzia ni juu ya mashamba.

Ruto Kipkemei: *Kingenyoru uhuru,*

Tlanslator:

Com. Abubakar Zein: Mzee wangu, asubuhi tulipoanza, tuliambia watu, historia ya Kenya sisi tunaifahamu vizuri, kuja kwa mzungu, kunyang'anywa kwa ardhi zetu, kupata uhuru, yote hayo tunayajua. Ngoja mzee wangu, wewe tupe mapendekezo yako tu, kile unataka tutie dani ya Katiba. Kama ni ardhi sema nataka ardhi hivi na hivi na hivi.

Ruto Kipkemei: *Amache imbare ne kiib serkali en forest kolenchon kiliboni*

Tlanslator: Kuna shamba ambalo serikali ilichukua kwa forest, nikaambia italipwa.

Ruto Kipkemei: *Kosir kole kikuren right holder.*

Tlanslator: Serikali ikaandikwa inaitwa right holder.

Ruto Kipkemei: *Kenyisiek sosom che kakosirto.*

Tlanslator: Miaka therathine zilizopita.

Ruto Kipkemei: *Ago ngunon togonye amache imbarenyun.*

Tlanslator: Mpaka sasa bado nangojea. Basi nahitaji shamba hili

Ruto Kipkemei: *Konyo koker imbarenon kwangen ole mi mbarenon kwa amache ameny imbarenyun.*

Tlanslator: Na nisipopata shamba ninajua mahali shamba liko na nitaenda kuishi.

Com. P. M. Wambua: Kuna watu walikuja hapa wakasema, shamba la mtu likichukuliwa na serikali kutumiwa kwa mambo ya public, yule ambaye alikuwa mwenye shamba apewe compensation, pesa ama apewe shamba lingine. Angelipenda hayo yafanyike?

Ruto Kipkemei: *Amache kou non keleliban, agot ndo kilibonon ko so so.*

Tlanslator: Nataka hivyo hivyo ata kama nilipwe au nipewe mahali pengine ni sawa.

Com. P. M. Wambua: Hiyo imeingia sasa. Aende kwa number la pili.

Ruto Kipkemei: *Ya pili awendi agobo kirwok.*

Tlanslator: Ya pili nataka kuguzia juu ya chiefs.

Ruto Kipkemei: *Ki keny ko kisirei raia kirwok.*

Tlanslator: Zamani raia walikuwa wakiandikisha machief.

Com. P. M. Wambua: Watu wengi walikuja hapa wakasema wanataka chiefs na assistant chiefs wawe wanachaguliwa na watu na wafanywe kwa mlolongo jinsi ilivyokuwa inafanywa hapo awali. Angelipenda hivyo?

Ruto Kipkemei: *Ko non.*

Tlanslator: Asante

Ruto Kipkemei: *Ko ya tatu, neso somok ko amache sukul somanet, amache kesoman kong'eten kilas nebo sisit agoi university ko ker serkali kole libandano, memuche bik kolipan.*

Tlanslator: Ya tatu nataka masomo shuleni

Com. P. M. Wambua: Kuna watu walikuja hapa wakasema wanataka elimu ipeanwe bure na serikali mpaka university. Hiyo iliingia?

Ruto Kipkemei: *Free agoi University.*

Tlanslator: Ni hivo, alikuwa anataka.

Com. P. M. Wambua: Angalia kwa karatasi kama kuna lingine. Chukua muda uangalie.

Ruto Kipkemei: *Kerichek.*

Tlanslator: Mambo ya madawa.

Com. P. M. Wambua: Kulikuwa na watu walikuja hapa wakasema wanataka ziwe bure kwa kila mkenya.

Ruto Kipkemei: *Nebo mwisho ko barabara.*

Tlanslator: Jambo la mwisho ni mabarabara.

Com. P. M. Wambua: Nilisikia hapa watu wanasema mabarabara yatengenezwe ndio wale watu ambao wako huko kwa mashinani wafikiwe – infrastructure ikataja. Atataka hivo ama anataka vingine? Mazao yao wauze kwa urahisi.

Ruto Kipkemei: *Kimoche kou non.*

Tlanslator: Atataka hivyo hivyo.

Ruto Kipkemei: *Nebo let ko komen.*

Tlanslator: Jambo la mwisho ni pombe. Nataka kukuuzia pombe.

Ruto Kipkemei: *Mi komen che kikosoror raini.*

Tlanslator: Na pombe ambayo imeingia wakati huyu.

Com. P. M. Wambua: Hiyo pia imetajwa. Kuna chupa dogo cha plastic zile whisky zile zinazwa haraka haraka ziondolewe zipigwe marufuku.

Ruto Kipkemei: *Chon che amache.*

Tlanslator: Hata hivyo akasema hata ile ya kienyenji pia ipigwe marufuku.

Com. P. M. Wambua: Basi, kwa hivyo tutapata wa mwisho ambaye ni rafiki yetu hapa. Na yeye pia atafupisha maneno manake nasikia ako na memorandum, lakini kwa record huwa atataja jina liingie kwa machine halafu utupatie kwa ufupi tu. Umesikia vile tumefanya, yale ambayo yametajwa yasirudiwe. Taja yale ya muhimu ambayo ni mapya halafu utupatie memorandum.

Nathaniel Barmotio: My names are Nathaniel Barmotio. Mainly I will touch on education. On free education there is a problem kwa hii mambo ya burseries. If possible we form a special unit in every district which will be seing into the burseries whether they have gone to the right children.

There is also the issue of format of taking students to colleges. In the former system when somebody was good in languages he could go directly for courses in languages. People who were good in science went for science but now the ministries are trying

to say that schools are doing very poor in languages and yet there are many students who are good in languages but they have given them restrictions. They may say they need somebody who will speak languages, who have passed in all the languages plus mathematics. What is the use of that mathematics and yet that person will not come and teach mathematics for life. So they should change the format that we should have colleges for languages and colleges for other pagadies for diploma and any other courses.

Lastly is what I'm shortening. I had done some others in the memorandum. Lastly because of the cost of life, you find that people are complaining on the issues of fees. One method, I was thinking that if possible we introduce day secondary schools so that our people will be able to pay their fees easily and people will be able to take their children to secondary schools by introduction of paying secondary school. Thanks.

Com. P. M. Wambua: Hayo kweli ni mafupi kabisa na yamefaa kwa hivyo asante sana jiadikishe hapa na utupatie memorandum. Kuna mtu hapa ambaye ako na mapya. I'm talking of new things which have not been said. Kwa hivyo huyu ataenda pale na akienda hapo ahakikishe yale ambayo ameyataja ni mapya. Tutayasikia hayo mapya. Shika hii na uendelee.

Philemon Kirui: Commissioners asante. Yangu ni mapya lakini sitasema mengi kwa sababu naona muda umeenda, saa imeenda, yangu tu ningependa kusema kwamba katika hii Katiba ya sasa ambaye Jina langu ni Philemon Kirui. Tume ya Katiba ya sasa isije tena ikafanya kosa kama ile ya mwaka ishirini na tatu ya Lanchaster. Hii shida tunayo sasa si ya leo, mambo ya Katiba ilikuwa Lanchasta 1963 na viongozi hapa Kenya walienda Lanchesta wakarudi na hiyo Katiba kutoka Lanchesta na kufika hapa sijui ile Katiba ilifanya namna gani. Na siyo ajabu, hata hii ya leo ikuwe kama ile ya Lanchesta.

Interjection

Com. P. M. Wambua: Ngoja kidogo Bwana Kirui, hio historia tunajua sana. Ile tunataka kusikia ni proposal. Utupatie proposal na iwe ni proposal mpya ambayo hatukuisikia tangu asubuhi.

Philemon Kirui: Asante, proposal yangu ni kuhusu ningependa kusema mimi naona kama saa imeenda ni ardhi na kortini na sheria. Mamulaka ya Rais ipunguzwe. Kenya iwe na waziri mkuu executive Prime Minister.

Kuhusu ardhi, sheria ya ardhi ipewe shula mpya kwa sababu sheria ya sasa imeruhusu unyakuzi wa ardhi.

Kuhusu ardhi, nchi zingine ardhi zimekuwa dogo lakini housing haijakuwa dogo. It is mandatory in Kenya that every person be provided with shelter, medicine, and food. Hapa Kenya, watu wa Kenya hawajui haya na ni vitu ambazo ni basic rights ya binadamu yeyote katika ulimwengu. Kenya we don't have such

Interjection

Com. P. M. Wambua: Philemon, wewe unapendekeza basic needs should be basic rights, in

Philemon Kirui: Yes, basic rights, that's what I mean.

Com. P. M. Wambua: including housing?

Philemon Kirui: Yes housing and water and shelter.

Com. P. M. Wambua: Una mengine mapya?

Philemon Kirui: Unajua naona kama mnaniharakisha sana. Sasa mimi naona tu nimalizane nayo kwa sababu saa imeenda.

Com. P. M. Wambua: Aaa, tunasema yale ambayo yamesemwa natukayaandika hakuna haja ya kurudia maanake sio hesabu tutafanya.

Philemon Kirui: So, ni mimi nimesema shelter, medical and What? And food. That is the basic right ya kila mtu kama wewe ni Mkenya.

Com. P. M. Wambua: Hiyo tumeandika dugu.

Philemon Kirui: Hiyo mmeandika? So, kuhusu mambo ya ardhi, nimesema kwamba the current land policy is weak. It has permitted what we call what? Corruption.

Com. P. M. Wambua: Na ukasema, Presidential powers zipunguzwe.

Philemon Kirui: Yes, Presidential powers should be reduced.

Com. P. M. Wambua: Zote tumeandika hizo.

Philemon Kirui: Yes, and then the country like Kenya, the future leadership should have a Prime Minister who is Executive. He should not be appointed. An appointed Prime Minister have problems because he works under somebody. So the Executive Prime Minister will have independent powers.

Ya mwisho ni judiciary – Legislature: Judiciary should be independent to empower to prosecute looters – people who loot our economy right away from the treasury. You loot today in Kenya, people loot our resources and then go with it. No court of law that says this person, if you have looted our economy you have looted our resources. You must be prosecuted but if judiciary is not independent, still under Executive President, then still we will have problems. We cannot manage to prosecute these people.

Com. P. M. Wambua: Kidogo, kwa sasa kuna judicial service commission ambayo inaappoint judges. These are the judicial service commission recompliment the appointment of the President, huwa ni Attorney General and Chief Justice yuko dani. Ungelipenda ku-rearrange hiyo mpango ndio iwe more independent ungepropose nini?

Philemon Kirui: I propose ya kwamba wawe wakisimamia wenyewe mambo ya sheria bila kuwa under Executive. Should be independent from what? From Executive.

Com. P. M. Wambua: Hiyo nimeweka sasa.

Philemon Kirui: I mean the chair is the President because the current judiciary is under the President. So what I mean should remain independent, s

Com. P. M. Wambua: Tumelewa sasa. Yenyewe mapya.

Philemon Kirui: Land transaction: The current land policy kwa sababu hainiluhusu unyaguzi wa ardhi, sheria ipewe jamii ili jamii wapewe ili jamii watawale utumishi pamoja na upanguzi kwa sababu saa hii kuna mtu mmoja ana shamba moja hapa moja

Eldoret, Nanyuki, Kitale, Mombasa. Hii mtu mmoja ataifanya nini?

Com. P. M. Wambua: Kidogo tafadhali, hiyo ilitajwa, na wakasema mambo yanaohusia mashamba yarudishwe kwa wananchi na village elders hao ndio wanaamua. On a _____ na kama kuna dispute. Na hiyo tumeandika.

Philemon Kirui: Kuhusu forestry, forestry ifiche ikae kwa mkono wa _____. Mimi nataka namna hii, I propose that forests and lakes should be handed over to United Nations because forestry ni kitu cha muhimu. Forestly goes also with _____. These are dangerous trends and most people will not understand the difficulties we are in because of the dipression of _____. If I say _____ from other people. But _____ the current climatical changes shows that the future will not be good. So forestly should be handed over to United Nations for protection and management. Okay Thank you very much.

Com. P. M. Wambua: Ngoja kidogo kuna swali kwa hiyo mambo ya UN. Kenya is a sovereign nation, we are sovereign people, hii ni nchi huru kabisa. Under what basis would you want to give a foreign body to control over our resources?

Philemon Kirui: Hapa Kenya tuna makabila albaine na nane and I know 42 tribes, sisi tukienda kama commission, tunaambiwa Marakwet haijahesabiwa, tunaambiwa watu hawajahesabiwa, lakini nasema kwa kabila yote 42 kila mtu kuchunga forest yake. This one will not be possible. Let me guide you this way, vile vitu zimetendeka hapa Kenya kutoka huko mbele haiwezi kuwa ni tofauti. Kenya ni nchi ambayo imewekwa na Mungu kulingana na ukabila yake ambayo siyo mbaya, its our heritage but still we cannot protect our forests as tribe based. No.

Com. P. M. Wambua: That's your view lakini kitu nilikuwa nataka kuestablish ni kwamba, the only thing which have really impressed me when I came to Baringo district is how you have looked at the environment, and if your justification for giving the people the right to land, you are saying that, because the people who live on that land _____ *tape unclear*. Then that same arguement can be used to say they can take care of the forest.

Philemon Kirui: No, no, what I mean is that there is land for – kama hii imekatwa, kama shamba za _____ and whatever.

Hiyo inagaiwa watu lakini forestry, ukipewa community, haitawezekana let me tell you this. People will tend to use forest as part of _____. So if we hand over to United Nations for protections, I plea it cannot be only Kenya. It has to be other countries which will support such a policy to protect our forests, to protect our indigeneous trees.

Com. P. M. Wambua: Tafadhali tumeelewa sasa. I think we take that as your proposal, except to register yourself. Na wewe ulizungumza jana, lakini ulizungumza jana. Haya ongezea lakini dakika moja tafadhali.

Aaron Kipchumba: Kwa majina ni Aaron Kipchumba. Ningependekeza ya kwamba parliament iwe na parmanent timetable, sio Rais anafikiria ni siku gani ataivuja na siku gani ataiamsha.

Ya pili ningependa wazazi wa watoto walio na ulemavu ambao hawawezi kusaidika wapewe social support.

Ya tatu ningependekeza ya kwamba wale waliona mahitaji ya kimatibabu ya maisha wapate matibabu hayo bila garama yeyote. Asante.

Com. P. M. Wambua: Jiandikishe hapo maanake tume... Ni kama tumemaliza sasa, nafikiri tumefika mwisho wa kikao hiki na ningependa kwanza kuwashukuru nyote ambao mmefika hapa na wale ambao tayari wameondoka maanake mulipima wakati na sasa ikiwa ni kama saa kumi hivi na dakika saba tumemaliza, na hiyo itatupatia muda nasi twende kujitayarisha kwa kikao cha kesho, nanyi mtarudi nyumbani mkaangalie ng'ombe, na nini ingine? Na kodoo, na buzi mhakikishe zimerudi nyumbani ama wamerudi nyumbani wakiwa wasalama. Kwa hivyo ningependa kuwashukuru nyote kwa niamba ya macommissioners wangu wawili ambao tayari wameondoka commissioner Mama Phoebe Asiyo na Commissioner Pastor Zablon Ayonga ambaye alikuwa mwenyekiti wa kikundi hiki na mwenzangu hapa ambaye tuko naye ambaye nitampa na nafasi naye pia azungumze kidogo, commissioner Zein. Tafadhalini kubali sisi tungependa kusema asanteni sana kwa kuja hapa kutoa maoni yenu. Maoni yenyewe yalikuwa yanafaa na mlipima wakati vizuri na tunataka kuhakikisha nyinyi kwamba yale maoni yote mliyatoa yataingia kwa Katiba. Tutakapofika kutengeneza report, tutahakikisha ya kwamba views presented to us, maoni

ambayo yalipeanwa na wananchi wote yameingia kwa hiyo report na tutatayarisha report kwanza ya constituency. Baringo North, wale ambao walikuja na walisema nini. Na hiyo report itarudishwa kwenu muiangalie, muichunguze mhakikishe ya kwamba kweli tulipofika huko Kabartonjo Chiefs Camp tulisema haya. Mtayakaguwa yale ambayo yatakuweco na kama kwa kweli kutakuwa na mengine ambayo hayakuandikwa na mliyasema, mtapewa na nafasi tena kusema haya tulisema hatukuyaona.

Vile vile kutakuwa na national report, na sheria ilioko inasema kwamba hiyo national report tutakapoitengeneza basi itarudishwa kwenu tena na pia mtaishoma. Ikiwa sheria haitapiduliwa, ikiwa sheria itakuwa vile bado ingali iko, report mtapewa muda muisome halafu mtatupatia maoni tena, halafu hiyo report tutaipeleka tena kwa national constitutional conference kikao cha kitaifa ambako kutakuwa na representatives kutoka Baringo districts, MP wenu ambao ni mjumbe atakuwa huko, nasi tutakuwa huko. Halafu tutazungumzia hiyo report tuangalie kweli kama itafaa Kenya. Tukisha kumbaliana, basi itapelekwa bunge na itapitishwa iwe Katiba mpya.

Ikiwa hatutakubaliana maanake kunawezekana tusikumbaliane, hawa wanasema hivi na wengine wanasema hivi, basi sheria ilioko sasa ikiwa ndio itakuweco, tutatakiwa tufanye referendum; wananchi waamue wenyewe. Waseme kwa wingi tunataka hivi. Kwa hivyo Katiba ambayo itatokea hapo mwisho, itakuwa kweli ni ile Katiba ya wananchi sio itakuwa Katiba ya commission, itakuwa ni wananchi maanake tumehakikisha ya kwamba kila stage wananchi wanakuwa involved. Kwa hivyo msije mkaona sasa tukitoka hapa mambo ya Katiba yameisha. Apana, tutarudi tena na hiyo report mtaletewa, mtapewa na nafasi ya kuisoma halafu mtahakikisha ya kwamba yale yote mlioyasema yako humo dani. Kwa hivyo tutarudi hapa na kutakuwa na nafasi nyingine tena lakini haitakuwa ya kupokea maoni kama jinsi mlivyofanya leo. Kwa hivyo kutoka hapa mkoa huu tutaenda Western. Ule mkoa ambao umebaki ni mmoja tu, Rift Valley na Western, tutamalizia huko Western na kulingana na programme ambao tumetayarisha, tutamaliza Western hapo mwisho wa mwezi huu wa saba. Halafu sasa tutaanza kutengeneza hiyo report. Kwa hivyo ikiwa vile tumepamba mambo hayabadiriki, tunafikiria tukifika hapa mwezi wa kumi pengine hizo reports zitakuwa tayari, na tutarudi hapa ndio mpewe na nafasi ya kuisoma na hivyo na hivyo. Lakini sheria ikibadilika basi tutawaeleza halafu tutajua jinsi tutavyoendelea. Kwa hivyo hiyo ndio sehemu ambayo inabakia kuanzia leo lakini kwa sasa tumefanya kazi nzuri na ningelipenda kuwashukuru na sana sana wale members wa 3Cs. Wako wapi? Kujeni hapa

tafadhalini.

Hawa wazee kama mnavyowaona, hawa ndio walikuwa wanashughulikia mambo ya civic education kuhakikisha ya kwamba mumefikiwa na materials, mmeleza jinsi tutakavyokuja kupokea maoni kuhakikisha ya kwamba maswala na maswali ambayo tutakuja hapa kuyasikiza na yale ambao mtatolea maoni yenu kweli imefanyika sawa sawa na kazi yao ilikuwa nzuri, hata nyinyi mtakumbali. Kwa hivyo kwa niaba ya tume ningelipenda kuwashukuru hawa members of 3Cs na district co-ordinator nafikiri hayuko hapa. Ako? Kuna muakirishi. Kwa hivyo kwa niaba ya tume, kwa niaba ya macommissioners ambao tulikuwa na wao hapa, kwa niaba ya tume nafikiria hao wakaaji wa hapa Baringo North Kabartonjo division, ile division nyingine ilikuwa inaitwa? Kipsalam. Kwa hivyo mtapokea shukurani zetu na hiyo kazi mliyofanya ni nzuri. Kwa ile stage ambayo imebakia tafadhalini mhakikishe ya kwamba kazi inaendeshwa tu vile mlifanya. Kwa hivyo kwa niaba ya tume asanteni sana. Na kabla sijasahau, tumemaliza hapo. Bwana DO provincial administration nasikia hapa kweli ilifanya kazi vizuri. Kwa hivyo kwa niaba ya tume pia, tafadhali pokea kwa niaba ya DC, Provincial Administration kwa ujumla upokee shukurani. Tutakupatia nafasi pia uzungumze yako, nafikiria tuko kwako utapata nafasi pia, useme machache. Nafikiria nitakoma hapo maanako yale yote ningelisema pengine tumeyasema na tumekubaliana tusirudie. Si ni kweli? Leo tumesema tusirudie maanake hamkurudia, na sisi hatutarudia, kwa hivyo nitamuuliza mwenzangu hapa aseme machache halafu tutamuuliza Bwana DO aseme machache halafu tutafunga kwa maobi maanake tuliaanza na maombi, halafu kikao tukifuje ama tukihailishe. Kwa hivyo

Com. Abubakar Zein: Yangu mafupi sana. Mimi ni kuwashukuru sana kwa kufika na kutoa maoni yenu vizuri sana na kutokea jana tumekuwa na siku nzuri jana na leo siku nzuri na tunawashukuru sana wakaazi wa Baringo North kwa kujitokesha kwa wingi na kutupa maoni ambao yanafaa na tunawahakikishia kwamba tutayatumia maoni haya kama mzingi wa kujenga Katiba yetu mpya kama tutavyotumia maoni ya Wakenya wengine katika sehemu zingine katika jamhuri yetu hii tukufu ya Kenya.

Pengine ambalo mwenzangu hakutaja na mimi ningependa kulitaja, ni kwamba jana yeye na mimi na wale macommissioners wengine tulipata fursa ya kukutana na yule mwenyeji wa Kipsalaman aliyekuwa ameishi million sita iliyopita. Kwa hivyo tulienda tukakutana na yeye huko, na sisi tukafurahi sana na badhi yetu tuna hadithi nyingi za kupeleka nyumbani kuwaelezea wazazi wetu pia kwamba tulikutana na mtu aliyeshi miaka million sita iliyopita huko pande za Lake Baringo, karibu na Lake Baringo.

Asanteni sana na Mungu awambaliki.

Na mwisho kabisa ningependa kusema kwamba tulipokuwa tukiendelea na kazi yetu, tulipata aalifa, we received information from the honourable member of parliament from this area giving his apologies that he had been held up at parliament due to important business in parliament today. Kwamba tulipata aalifa kutoka kwa mbunge mheshimiwa Kiptuni wa area hii kwamba ameshikika na kazi bungeni leo na akaomba watu wamuie ladhi kwamba hakuweza kuwa na sisi hivi leo. Na sisi tulikubali hivyo na tukasema, kabla hatujaondoka tutawaelezea mambo tulioalifiwa sisi. Asanteni sana.

Com. P. M. Wambua: Huyo rafiki yetu alitajwa na commissioner Zein hakutupatia maoni maanake hali yake ni ile hawezi kutoa maoni lakini tulisoma na tukachukua maoni kutoka huko. Kitu kingine ambacho pengine ningelitaja ambacho Bwana DO amenikubusha ni kwamba ikiwa umekosa na nafasi ama mtu mwingine amekosa na nafasi ya kutoa maoni leo, baado kuna nafasi. Anaweza kuandika maoni yake na apatie district coordinator ama one of the members of the 3Cs na hayo yatatufikia huko Nairobi na tutahakikisha ya kwamba yataingia kwa ile orodha na tutafanya analysis. Kwa hivyo usione kama ni mwisho. Ikiwa kuna mtu alikosa na nafasi kuja leo, anaweza kuandika halafu apeane na ikija huko itaingia kwa ile orodha ya wale ambao wametupatia maoni.

Ya pili, ikiwa unaweza kufika pengine neighbouring constituency maanake tuko hapa tu, kesho tuko Baringo Central hapo Kabarnet. Ukiwa unaweza kujisqeeze, pengine uamke mapema, uwe mbele, pengine tunaweza kukusikia. Lakini ukifika huko ikiwa watu wameandika na hautafikiwa na nafasi, bado bado nafasi iko utaandika maoni utuletee. Kwa hivyo hayo ndio nilikuwa nataka kusema maanake nimekubushwa na bwana DO. Kwa hivyo Bwana DO unaweza kusema machache halafu tufunge kikao.

D.O.: Basi langu ni kuwashukuru kwa hii kazi ambayo imefanyika tangu jana mpaka leo. Vile mwenyekiti wa kikao hiki saa hizi amesema, mumeona mwenzetu Aaron Kipchumba, jana alikuwa Kipsalaman, kuna kitu alisahau, unaona amepatiwa nafasi? So kwa hivyo vile vile amesema ikiwa leo umepata shida lingine, still you can present at Kabarnet kesho. Sitaki kuchukuwa wakati mwingi, langu tu ni kushukuru wakaaji wa area hii, constituency ya Baringo North kutokea jana mpaka leo mumeweka

amani katika kikao hiki ambacho kimefanyika siku ya leo, na hapa Kabartonjo tumefanyia nje mahali ambapo kila mtu alipata nafasi yake kutoa maoni yake. Tungefanyia dani ya hall lakini tuliangalia ya kwamba wacha tuje nje mahali kila mtu ako na huru kutoa maoni yake. Kwa hivyo nashukuru nasema asanteni.

Com. P. M. Wambua: Tumpate mtu mmoja atuombee.

Speaker: Tutasimama zote. Basi natuombe, Mungu Jehova Baba wa bingu, asante baba kwa sababu ya wema wako, asante kwa ajiri ya msaada ambao umetupa, twaungama wazi ya kwamba, kama si wewe hatungeweza kufikia mahali ambayo tumefika. Asante kwa kila jambo ambayo ilifanyika tangu jana tulipokuwa kule Kipsalaman mpaka hata na leo tumekuwa hapa Kabartonjo, twakushukuru Mungu Baba kwa ajiri ya amani, twakushukuru Mungu baba kwa ajiri ya yote mema ambayo umefanya kwa ajiri yetu. Hata kwa ajiri ya maandishi, mazungumzo yale yote ambayo tumeyazungumzia kuhusu nchi yetu, baba tunakuhitaji na tunakuita ya kwamba kila jambo na kila kato ambalo litakatwo na wanakenya lipate kutufaa na kufaa hata na wale ambao watatufuata baadaye. Uibariki nchi hii, uibariki kila mmoja iishie katika nchi hii na hata kwa siku sijazo baraka hizo zipate kuandamana pamoja nasi. Asante Mungu kwa ajiri ya wageni ambao wametutembelea, wanaporudi manyumbani mwao au mahali ambao wataenda kikazi uwabariki uwasaidie wapate kuona uzuri wako na uzuri wa kuwa pamoja na Mungu. Baba tena wale watabaki wawe chini ya neema yako, utubariki tunapokaa, hata wanapoondoka uwe pamoja nasi. Twakushukuru kwa hayo machache kwa jina la Yesu ambaye ni mwokozi wetu. **Amen.**